**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

# RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA USTAWI WA JAMII YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**FEBRUARI, 2024**

**YALIYOMO**


SEHEMU YA KWANZA........................................................................................................1

1.0 UTANGULIZI ..........................................................................................................1

1.2 MUUNDO WA KAMATI ...........................................................................................2

1.3 MALENGO YA KAZI NA MUDA WA KAZI ZA KAMATI .......................................3

1.4 HADIDU REJEA .........................................................................................................3

SEHEMU YA PILI ..............................................................................................................4

2.0 WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA MAFUNZO YA AMALI ..........................4

2.1 IDARA ........................................................................................................................4

2.2 MABARAZA NA BODI .............................................................................................4

2.3 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ..............................................................................4

1. PROGRAMU YA ELIMU YA JUU.............................................................................5

A. CHUO KIKUU CHA SUZA.........................................................................................6

CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR (SUZA) ...........................................................................................................................7

MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI ..............................................8

CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SKULI YA SAYANSI BENJAMIN WILLIAM MKAPA TAWI LA SUZA PEMBA.............................................................................10

MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI ............................................11

B. BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU.................................................................11

CHANGAMOTO INAZOZIKABILI BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU ZANZIBAR..................................................................................................................12

MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI ............................................12

2. PROGRAMU KUU YA ELIMU YA SEKONDARI....................................................13

A. SKULI YA SEKONDARI YA UFUNDI .....................................................................14

CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SKULI YA SEKONDARI YA UFUNDI MIKUNGUNI ...............................................................................................................14

MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI................................................14

B. CHUO CHA KIISLAMU UNGUJA ............................................................................16

CHANGAMOTO ZINAZOZIKABILI CHUO CHA KIISLAMU UNGUJA ....................16

MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI ............................................17

3. PROGRAMU YA UBORA WA ELIMU.......................................................................18

A. TAASISI YA ELIMU.................................................................................................19

CHANGAMOTO ..........................................................................................................19

MAONI /USHAURI WA KAMATI ........................................................................................19
B. OFISI YA MKAGUZI MKUU WA ELIMU ZANZIBAR .........................................20
CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI OFISI YA MKAGUZI MKUU WA ELIMU ZANZIBAR ..............................................................................................................................20
MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI ..........................................21
C. BODI YA HUDUMA ZA MAKTABA ZANZIBAR.............................................22
CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI BODI YA HUDUMA ZA MAKTABA. .............23
MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI ..........................................23
(D) BARAZA LA MITIHANI ..........................................................................................24
CHANGAMOTO ZINAZOZIKABILI BARAZA LA MITIHANI ZANZIBAR ...........24
MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI ..........................................24
4. PROGRAMU KUU YA ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI ........25
CHANGAMOTO ...............................................................................................................25
MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI ..........................................25
5. PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI..............................................................................................26
CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI ....................................................................................................................................26
MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI ..........................................28
SEHEMU YA TATU..............................................................................................................30
3.0 WIZARA YA AFYA .......................................................................................................30
IDARA....................................................................................................................................30
TAASISI .................................................................................................................................30
MABARAZA YA KITAALUMA/BODI .........................................................................30
1. PROGRAMU KUU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA(PHO1) ..........................31
A. ZIARA YA KAMATI KITUO CHA AFYA RAHALEO .......................................32
CHANGAMOTO ...............................................................................................................32
USHAURI /MAONI YA KAMATI ..................................................................................32
2. PROGRAMU KUU YA TIBA .......................................................................................33
A. WAKALA WA BOHARI KUU YA DAWA ZANZIBAR ......................................33
CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WAKALA WA BOHARI KUU YA DAWA......34
MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI ..........................................34
B. MFAMASIA MKUU WA SERIKALI .........................................................................36
CHANGAMOTO ...............................................................................................................37

USHAURI/MAONI YA KAMATI ..... 37
C. TAASISI YA UTAFITI WA AFYA ZANZIBAR (ZAHRI) ..... 38
CHANGAMOTO ZA TAASISI YA UTAFITI WA AFYA ZANZIBAR (ZAHRI) ..... 38
MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI ..... 39
(D) WAKALA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI ..... 40
CHANGAMOTO ..... 40
USHAURI/MAONI YA KAMATI ..... 40
(E) WAKALA WA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI ..... 41
USHAURI /MAONI YA KAMATI ..... 41
(F) ZIARA YA KAMATI HOSPITALI YA KIVUNGE ..... 42
CHANGAMOTO ..... 42
USHAURI/MAONI YA KAMATI ..... 43
3. PROGRAMU KUU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA ..... 43
CHANGAMOTO ..... 44
USHAURI/MAONI YA KAMATI ..... 45
 ZIARA YA KAMATI KATIKA DIVISHENI YA AFYA YA AKILI HOSPITALI YA KIDONGO CHEKUNDU ..... 46
CHANGAMOTO -- DIVISHENI YA AFYA YA AKILI KATIKA HOSPITALI YA KIDONGO CHEKUNDU ..... 46
MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI ..... 47
4. PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI WA URATIBU WA WIZARA ..... 49
CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WIZARA YA AFYA KWA UJUMLA ..... 49
MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI ..... 52
UTEKELEZAJI ..... 54
Matumizi ..... 55
Hali ya Kifedha kwa upande wa Hospitali ya Mnazi Mmoja(H02), ..... 55
Mapato ..... 56
SEHEMU YA NNE ..... 57
4.0 WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO ..... 57
UPATIKANAJI WA FEDHA ..... 58
UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ..... 59
1. PROGRAMU YA HIFADHI YA JAMII (PH0401) ..... 59
CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ..... 59
MAONI /USHAURI WA KAMATI. ..... 59

2. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA (PH0402) ............60
CHANGAMOTO ............61
MAONI/USHAURI WA KAMATI ............61
3. PROGRAMU YA MAENDELEO YA JAMII NA JINSIA (PH0403) ............62
CHANGAMOTO............63
MAONI /USHAURI /MAPENDEKEZO YA KAMATI ............64
SEHEMU YA TANO ............66
5.0 WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO............66
SEKTA YA HABARI ............66
SEKTA YA VIJANA ............66
SEKTA YA UTAMADUNI............66
SEKTA YA MICHEZO ............66
1. PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA HABARI, UTANGAZAJI NA UCHAPAJI............67
A. SHIRIKA LA MAGAZETI ZANZIBAR (SMS) ............68
MAONI YA KAMATI/USHAURI WA KAMATI ............70
B. WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR (ZAGPA)............70
CHANGAMOTO KATIKA WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR 71
MAONI/USHAURI /MAPENDEKEZO YA KAMATI. ............71
C. SHIRIKA LA UTANGAZAJI LA -ZBC ............71
CHANGAMOTO ZA SHIRIKA LA UTANGAZAJI LA ZBC ............72
MAONI /USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI. ............72
2. PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO............73
A. BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA ZANZIBAR............74
CHANGAMOTO ZINAZOLIKABILI BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA ZANZIBAR. ............74
MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI ............74
B. BARAZA LA SANAA, SENSA YA FILAMU NA UTAMADUNI............75
CHANGAMOTO ZA BARAZA LA SANAA SENSA YA FILAMU NA UTAMUDUNI 76
MAONI YA KAMATI/USHAURI WA KAMATI ............76
C. ZIARA YA KAMATI KATIKA Mradi wa Ukarabati wa Uwanja wa Amaani- Unguja 76

CHANGAMOTO ZA MRADI WA UKARABATI UWANJA WA AMANI ................77
MAONI YA KAMATI/USHAURI KWA UWANJA WA AMANI ...............................77
CHANGAMOTO ZA UKARABATI NA UBORESHAJI WA UWANJA WA GOMBANI PEMBA ....................................................................................................79
MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI ............................................79
3. PROGARAMU KUU YA MAENDELEO YA VIJANA (PJ0302...........................79
CHANGAMOTO ..........................................................................................................80
MAONI/USHAURI WA KAMATI ..................................................................................80
4. PROGRAMU KUU YA UTAWALA NA UENDESHAJI WA WIZARA(PJ0304)80
CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO ..............................................................................................................81
MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI ............................................82
SEHEMU YA SITA ......................................................................................................83
6.0 HITIMISHO..............................................................................................................83

# SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Zanzibar iliyoanzishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 85 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na Kanuni ya 107(1) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, (Toleo la 2020).

Kazi na majukumu ya Kamati hii yameelezwa na kufafanuliwa kwenye Jadweli la Kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo:

*(a)* Kufuatilia utekelezaji wa Maagizo ya Kamati yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia;

*(b)* kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji wa Bajeti na hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza;

*(c)* Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi katika Wizara husika;

*(d)* Kuchunguza na kufuatilia Mapato na Matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha;

*(e)* Kuchambua Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Wizara husika ya Mapato na Matumizi ya kila mwaka;

*(f)* kushughulikia Miswada ya Sheria inayokabidhiwa kwake na Spika;

*(g)* Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekeleaji wa ahadi hizo; na

*(h)* Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Kamati ya Kudumu ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, katika Ripoti hii inajulikana kama "Kamati" ambapo ina jukumu la kufuatilia utekelezaji wa Wizara nne (4) za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ikiwa ni pamoja na Idara, Mashirika, Wakala, Mabaraza na Vitengo vilivyo chini ya Wizara hizo. Wizara hizo ni :

*(a)* Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali;

*(b)* Wizara ya Afya;

*(c)* Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; na

*(d)* Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

## 1.2 MUUNDO WA KAMATI

Kamati hii inaundwa na Wajumbe wafuatao:

| **Nam.** | **Jina** | **Wadhifa** |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Sabiha Filfil Thani | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Nassor Salim Ali | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Abdalla Hussein Kombo | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Haji Omar Kheri | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Salma Mussa Bilal Mhe. | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Sulubu Kidongo Amour | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Bahati Khamis Kombo | Mjumbe |

Aidha, Kamati hii inafanya kazi zake kwa kushirikiana na Makatibu wafuatao:

| **Nam.** | **Jina** | **Wadhifa** |
|---|---|---|
| **1.** | Ndg. Talib Enzi Talib | Katibu |
| **2.** | Ndg. Salha Abdulla Abdulla | Katibu |
| **3.** | Ndg. Bakar Makame Haji | Katibu |

### 1.3 MALENGO YA KAZI NA MUDA WA KAZI ZA KAMATI

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Kamati ilitekeleza kazi zake kwa malengo yafuatayo:

(a) Kufuatilia Maagizo yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka 2022/2023.

(b) Kufuatilia ahadi za Serikali zilizotolewa katika Mkutano wa Bajeti wa mwaka 2023/2024.

(c) Kufuatilia utekelezaji wa Bajeti (kazi za kawaida na kazi za maendeleo) ya mwaka 2023/2024.

(d) Kufanya ziara katika maeneo na taasisi husika.

Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Kamati ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki Sita kama ifuatavyo:

(i) Tarehe 14/08/2023 hadi tarehe 18/08/2023 kwa upande wa Pemba na kuanzia tarehe 21/08/2023 hadi tarehe 25/08/2023 kwa upande wa Unguja.

(ii) Tarehe 06/11/2023 hadi tarehe 10/11/2022 kwa upande wa Pemba na kuanzia tarehe 13/11/2022 hadi tarehe 17/08/2022 kwa upande wa Unguja.

(iii) Tarehe 15/01/2023 hadi tarehe 19/01/2023 Unguja na kuanzia taerehe 22/01/2023 hadi tarehe 26/01/2023 Unguja.

### 1.4 HADIDU REJEA

Katika Utekelezaji wa kazi kwa mwaka 2023/2024, Kamati ilitumia hadidu rejea zifuatazo:

(a) Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Toleo la Mwaka 2020;

(b) Taarifa Rasmi za Baraza 'Hansard' za Baraza za Mwaka 2023/2024;

(c) Ripoti za Kamati kwa Mwaka 2022/2023;

(d) Hotuba za Bajeti za Taasisi za Serikali zinazosimamiwa na Kamati hii.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA MAFUNZO YA AMALI

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Mafunzo ya Amali inaundwa na Idara Saba (7), Mabaraza Matatu (3), Bodi Tano (5) pamoja na Ofisi mbili (2) kama ifuatavyo:

### 2.1 IDARA

(i) Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
(ii) Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
(iii) Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi;
(iv) Idara ya Elimu ya Sekondari;
(v) Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima;
(vi) Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu;
(vii) Idara ya Michezo na Utamaduni katika Elimu; na
(viii) Ofisi Kuu Pemba.

### 2.2 MABARAZA NA BODI

(i) Baraza la Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia;
(ii) Baraza la Mitihani Zanzibar;
(iii) Baraza la Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar
(iv) Bodi ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali;
(v) Bodi ya Taasisi ya Elimu Zanzibar;
(vi) Bodi ya Huduma za Maktaba;
(vii) Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu; na
(viii) Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu.

### 2.3 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU

Mpango kazi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali unatekelezwa kupitia programu sita kama ifuatavyo:

Programu ya 1: Elimu ya Maandalizi na Msingi

Programu ya 2: Elimu ya Sekondari.

Programu ya 3: Elimu ya Juu

Programu ya 4: Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali

Programu ya 5: Ubora wa Elimu

Programu ya 6: Uongozi na Utawa

Programu hizi za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali zinatekelezwa kwa mashirikiano makubwa ya utatu, yaani baina ya Serikali, wananchi, washirika tofauti wa maendeleo wa ndani na nje.

Pamoja na Programu hizo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pia kuna Miradi Mitano (5), ambayo ni hii ifuatayo:

(i) Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi na Elimu ya Msingi;
(ii) Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Lazima;
(iii) Mradi wa Uimarishaji wa Elimu Mbadala na Amali; na
(iv) Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu katika Elimu.
(v) Mradi wa uimarishaji wa Elimu ya Juu

Kamati katika utekelezaji wa kazi zake iliweza kufuatilia utekelezaji wa Programu za Wizara kama ifuatavyo:

## 1. PROGRAMU YA ELIMU YA JUU

Programu hii ina lengo la kutoa elimu itakayomuwezesha mhitimu kujiajiri au kuajiriwa. Progamu hii ina programu ndogo moja ambayo ni mafunzo ya ualimu na maeneo manne ya huduma; ikiwemo Huduma ya Ushauri na Utafiti, Huduma ya Sayansi na Teknolojia, Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu na Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu.

Katika mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya shilingi 58,724,112,000/= zimepangwa kutumika katika Programmu hii

Jumla ya TZS 34,109,914,851/- zilipangwa kutumika katika kipindi cha Julai – Disemba, 2023 ambapo TZS 25,112,008,184/- sawa na asilimia 74 zilipatikana.

a) Aidha, Taasisi imefanya matengenezo ya kawaida kwa majengo mengine yakiwemo majengo ya utawala na jengo la TEHAMA.

b) Wizara, Katika jitihada za kuongeza wataalamu wa ufundi nchini, imekamilisha matayarisho ya uanzishwaji wa program mpya mbili kwa mwaka wa masomo 2023/2024 katika taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia. (KIST). Program hizo ni Stashahada ya Ualimu Ufundi na Stashahada ya Ufundi wa Vifaa tiba.

Kamati imeweza kufuatilia utekelezaji wa Programu za Wizara katika taasisi zake kama ifuatavyo:

### A. CHUO KIKUU CHA SUZA

Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) ni Chuo Kikuu pekee cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Chuo kilianzishwa chini ya Sheria Nam. 8 ya mwaka 1999 sambamba na marekebisho ya Sheria ya Chuo, Nam. 11 ya mwaka 2009. Aidha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipitisha Sheria ya Mabadiliko ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar Nam. 7 ya mwaka 2016, ambapo Sheria hiyo ilifuta Sheria zilizoanzisha Chuo cha Uongozi wa Fedha - Chwaka (ZIFA), Chuo cha Taaluma za Afya - Mbweni na Taasisi ya Maendeleo ya Utalii - Maruhubi (ZIToD).

Vile vile, kuanzia mwaka wa fedha 2019/2020 Serikali iliridhia kuunganisha Taasisi ya Chuo cha Teknolojia ya Kilimo - Kizimbani (KATI) kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na kuwa Skuli ya Kilimo ya Chuo Kikuu cha

Taifa cha Zanzibar. Sambamba na hilo, katika mwaka huo huo wa fedha 2019/2020 Serikali pia ilianzisha Skuli Mpya ya Utibabu wa Meno ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Chuo kimeanzisha Skuli Mpya ya Kompyuta, Mawasiliano na Taaluma za Habari, Skuli hii inatokana na kuunganishwa kilichokuwa Chuo cha Uandishi wa Habari Zanzibar na kuwa sehemu ya SUZA mwaka 2020, ambapo mabadiliko hayo yamapelekea ukuaji mkubwa wa Chuo.

Vile vile, Chuo hiki kinatekeleza shughuli zake kuu za msingi ambazo ni kufundisha, kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaaluma. Chuo kina miaka 21 tangu kianzishwa kwake na kinafundisha programu 67 katika ngazi za Shahada ya Uzamivu, Shahada ya Uzamili, Shahada ya Kwanza, Stashahada na Cheti.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR (SUZA)**

(a) Uendeshaji wa Mfumo wa pamoja wa vyuo na taasisi zilizo chini ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar –SUZA ambao unadaiwa kuwa na changamoto mbali mbali.

(b) Matumizi ya Mfumo Mpya wa Manunuzi umeleta changamoto ya kuchelewesha kupatikana Wazabuni wa Miradi na Manunuzi ya Chuo.

(c) Mishahara midogo ya SUZA kulinganisha na vyuo au Taasisi nyengine, hii inapelekea wanataaluma wengi kuchukua likizo bila ya malipo kwa ajili kutafuta maslahi yaliyobora nje ya Chuo.

(d) Uhaba wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia yenye kukidhi uhitaji halisi uliopo kwa Kampasi zote za Chuo. Kozi za Sayansi Asilia, Kilimo pamoja na Afya zinauhitaji mkubwa wa vifaa vya maabara, kemikali pamoja na vitenganishi ambavyo vinahitaji gharama kubwa kuvinunua na kuvihifadhi. Chuo hulazimika baadhi ya muda kutumia maabara za nje ya Chuo kwa ajili ya kuendesha mafunzo kwa vitendo.

(e) Upungufu wa wahadhiri wa ngazi zote unaopelekea kutegemea zaidi walimu wa muda (part timers). Kwa sasa Chuo hulazimika kutumia gharama kubwa ya mapato ya ndani kwa ajili ya malipo ya walimu wa muda. Pia Chuo kinakabiliwa na tatizo la wahadhiri wenye sifa wanaoendana na vigezo vya Chuo Kikuu. Suala hili linatokana na Chuo kurithi baadhi ya walimu ambao hawana vigezo vinavyotambulika na TCU;

(f) Uhitaji mkubwa wa ukarabati wa miundombinu kutokana na uchakavu wa majengo karibu kila Kampasi ya Chuo. Chuo kimerithi majengo mengi ambayo yamechakaa na yanahitaji gharama kubwa kuyatengeneza. Chuo kinaendelea kutenga fedha kidogo kidogo kwa ajili ya ukarabati ambao haukidhi haja ya mahitaji yaliopo.

(g) Uchache wa vifaa vya kufundishia kama vile kompyuta karibu kila kampasi ya Chuo. Studio ya Redio pamoja na Kituo cha Mafunzo ya Kidigitali navyo vinakabiliwa na upungufu wa vifaa.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inaishauri serikali kuharakisha kutoa maelekezo kuhusu Mpango wa mageuzi ya Chuo KIKUU CHA SUZA katika uendeshaji wa Taasisi zake ili kuweka sawa Mfumo wa Ugatuzi unaoendelea ambao umeviunganisha vyuo mbali mbali na Suza. Kamati inapongeza hatua hiyo kwa vile utekelezaji wa mfumo huo wa ugatuzi uliopo umekua na madai ya changamoto mbali mbali kutoka kwa taasisi zilizounganishwa na SUZA.

(b) Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuwapatia vibali vya ajira Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kila inapohitajika kwa ajili ya kuajiri wafanyakazi wapya ili kupunguza nakisi ya wafanyakazi wa muda ambao wanatumia fedha nyingi za Serikali na pia kuwaboreshea

maslahi wahadhiri ili kuepuka kuhama na kwenda vyuo vyengine kwa kufuata maslahi.

(c) Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuwaongezea bajeti ya mishahara Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) ili wafanyakazi waweze kufanya kazi kwa ufanisi na kuondokana na dhana ya kutafuta maslahi bora katika vyuo vya nje.

(d) Kamati pia inaishauri Serikali kuwatengea bajeti ya maendeleo kwa ajili ya kujenga miundombinu mipya pamoja na kufanya ukarabati mkubwa wa majengo katika kampasi zake zote zinazosimamiwa na Uongozi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA).

(e) Kamati inaishauri kwa Serikali kupitia Tume ya Mipango Zanzibar kutenga bajeti maalum kwa ajili ya kukiendeleza Chuo Kikuu kwa upatikanaji wa vifaa vya kisasa katika maabara zetu kwa lengo la kutoa wahitimu waliobobea katika fani zinazohitajika kwa maendeleo endelevu ya Taifa hili.

(f) KAMATI inaishauri serikali kupitia malipo ya ada ya chuo ambayo yameonekana ni makubwa, hali iliyopelekea kukosekana kwa wanafunzi 70 waliotarajiwa kujiunga na chuo na kupatikana 46 kwa mwaka wa mwanzo wa masomo 2023.

(g) Kamati inaishauri Wizara kupitia SUZA kuwa na mpango wa kimkakati wa kusaidia kuendeleza Maabara ya ubunifu ya **WasteX lab** badala ya kuwaachia wafadhili pekee. Programu hiyo ya ubunifu inayofadhiliwa na shirika la UNICEF na UNDP inalenga kuunganisha bunifu zinazohusiana na uchakataji wa taka ngumu kwa kutumia mbinu ijulikanao kama uchumi mzunguko (circular economy) ambao uanzilishi huo umeanzisha kituo cha uweledi (Centre of excellence) kinachokusanya makundi tofauti ya wataalamu, ambao wanatumia vifaa na huduma zilizomo kwa taasisi tofauti ambazo zonajihusisha na masuala ya uongozi, tafiti, usaidizi na mafunzo.

(h) Kamati inaishauri wizara kupitia SUZA kuwa na data base maalum ambayo itakusanya Tafiti mbali mbali ambazo zimefanywa na chuo na kuweza kuhifadhiwa ili ziweze kusaidia katika shughuli mbali mbali za maendeleo nchini.

(i) Aidha Kmati inashauri Chuo kikuu cha Taifa SUZA kuendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi wake wote katika kozi fupi fupi, ndani na nje ya Zanzibar katika fani mbali mbali zikiwemo Uchumi wa bluu, Mafuta na gezi, Uhasibu, Ukaguzi, Ukutubi, Kutunza rikodi na fani nyenginezo.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SKULI YA SAYANSI BENJAMIN WILLIAM MKAPA TAWI LA SUZA PEMBA**

(a) Upungufu wa wahadhiri wakudumu, Kampasi bado inategemea kutumia walimu wa muda kufundisha masomo mbali mbali.

(b) Ukosefu wa uzio katika eneo la Skuli ya Sayansi Benjamin William Mkapa, hali inayopelekea uvamizi wa maeneo ya Skuli kwa shughuli za kijamii ikiwemo wanyama kufungwa ndani ya eneo pamoja na wanajamii kupita katikati ya eneo la Skuli hiyo.

(c) Uhaba wa rasilimali watu pamoja na vitendeakazi katika Skuli ya Sayansi, hali inayosababisha kupungua ufanisi wa utendaji kazi katika Skuli hiyo.

(d) Ukosefu wa Kituo cha Afya katika mazingira ya Skuli, hali inayosababisha kuwapa wakati mgumu wanafunzi wa skuli hiyo pale wanapopata matatizo ya kiafya hasa wakati wa usiku.

(e) Ukomo wa matumizi ya fedha kwa Skuli hiyo baada ya kuunganishwa na SUZA, hali inayozorotesha utekelezaji wa baadhi ya majukumu ya Skuli na kutofikia malengo iliyojipangia kwa wakati.

(f) Uhitaji mkubwa wa ukarabati wa miundo mbinu ambapo hali ya majengo hairidhishi licha ya kuwa si ya muda mrefu haikidhi mahitaji ya matumizi yaliyopo
(g) ukosefu wa usafiri wa kudumu kwa walimu na wanafunzi wa Skuli hiyo hali inayosababisha walimu kuchelewa kuanza kwa vipindi vya masomo kwa wakati.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inaushauri Uongozi wa Chuo Kikuu cha Taifa SUZA kuimarisha miundo mbinu ya skuli ya Benjamin Mkapa pamoja na kukamilisha mpango wake wa kujenga uzio katika Skuli hiyo kwa ajili ya kuwa na mazingira rafiki ya kujifunzia na kufundishia.
(b) Kamati inaishauri kwa Uongozi wa Chuo Kikuu cha Taifa SUZA kuajiri Wakufunzi wenye uwezo pamoja na sifa katika Skuli ya Sayansi Benjamin William Mkapa Tawi la SUZA Pemba, kwa ajili ya kuweza kusomesha wanafunzi wa kada mbali mbali ili kupunguza kuchukua walimu wa muda nje ya skuli.
(c) Kamati inaushauri Uongozi wa Chuo Kikuu cha Taifa SUZA kuipatia Skuli ya Sayansi ya Benjamin William Mkapa Tawi la SUZA Pemba vifaa vya kisasa vya kujifunzia na kufundishia, ili waweze kwenda sambamba na kasi za mabadiliko ya elimu duniani.
(d) Kamati inashauri Wizara kufanya utafiti kuhusu wahitimu wa Skuli ya MKAPA ili kuona wanafunzi hao wanakubalika katika soko la ajira katika sekta ya ualimu iliyopo.

**B. BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU**

Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar ni imeanzishwa miaka 13 iliyopita chini ya Sheria Namb.3/2011 ikiwa na majukumu makuu yafuatayo:

- Kutoa mikopo ya kugharamia elimu ya juu kwa wanafunzi
- Kufuatilia marejesho ya mikopo ya elimu ya juu kwa wahitimu
- Kutafuta nafasi ya ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi .
- Kutoa Scholarship kwa vyuo vya ndani zinazotolewa na SMZ kwa wanafunzu wenye ufaulu mzuri wa Daraja la kwanza katika mitihani ya kidato cha sita.

Taasisi ilitengewa Bajeti ya TZS 14.5 Bilioni katika kipindi cha miezi sita ambapo kati ya hizo mikopo ya wanafunzi ni TZS 13.45 Bilioni na gharama za uendeshaji ofisi ni TZS 1.05 Bilioni.

Miongoni mwa malengo ya mwaka ya Bodi ni:

- kutoa mikopo kwa wanafunzi 6,060 wahitaji wa kujiunga na elimu ya juu.
- Kukusanya madeni TZS 4.09 Bilioni kutoka katika vyanzo vya ndani vya BMEJZ

**CHANGAMOTO INAZOZIKABILI BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU ZANZIBAR**

- Kuchelelwa kupatikana kwa fedha za mikopo ili kuweza kuwalipa mapema wanafunzi vyuo vinapofunguliwa.
- Utafutaji wa vyanzo vipya vya mapato ya Bodi baada ya kodi ya Skill Develepment Levy kuondolewa na SMZ
- Kupatikana kwa jengo la kudumu la Bodi Unguja na Pemba
- Ongezeko la wanafunzi wanaohitajikusoma nje ya nchi
- Kupatikana kwa Gawio la fedha za Mikopo kutoka SMT /HESLB kwa ajili ya Zanzibar

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

- Kamati inaishauri Serikali kwa kuongeza BAJETI ya Mikopo ya wanafunzi kutoka TZS 19.50 Bilioni kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na kufikia TZS 29.05 Bilioni katika mwaka wa masomo 2023/2024

- Kamati inaishauri Wizara/Bodi ya Mikopo kuhakikisha wanaendeleza utaratibu wa **Top up tuition fee** kwa wanafunzi wanaopatiwa mikopo pungufu ya elimu ya juu kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya SMT(HESLB)
- Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Makamo wa pili wa Rais kulifatilia suala la Zanzibar kupatiwa Gawio la fedha za Mikopo kutoka SMT/HESLB kwa vile suala hilo limeonekana kuwa ni la kisera zaidi ambapo mazingatio na utekelezaji wake unahitaji mazungumzo ya kati ya Serikali ya SMZ na SMT. Kamati imebaini kuwa iwapo Zanzibar itapatiwa gawio hilo la fedha la asilimia 10 ya Bajeti ya HESLB itaweza kupata zaidi TZS Bilioni 70 ambazo zitakidhi haja katika kutoa mikopo ya kugharamia elimu ya juu kwa wahitibu wa vyuo wa Zanziba

## 2. PROGRAMU KUU YA ELIMU YA SEKONDARI

Programu hii ina lenga kutoa na kuimarisha Elimu ya Sekondari kwa kuhakikisha vifaa vya maabara na kemikali kwa ajili ya mitihani ya taifa kwa skuli zote za Sekondari zenye kidatu cha nne, tano na sita vinanunuliwa na kusambazwa katika skuli hizo.

Programu hii kwa mwaka 2023/2024 imepangiwa kutumia jumla ya Tanzania shilingi bilioni mia moja na themanini na tisa, milioni mia tisa na sabini na mbili, laki moja na elfu kumi na mbili (189,972,112,000/=). Kwa kipindi cha Julai – Disemba, 2023 programu hii ilipangiwa jumla ya TZS. 90,930,221,664/=. Hadi kufikia Disemba 2023, jumla ya TZS. 90,143,243,046/= sawa na asilimia 99 zilipatikana. Kamati katika ufuatiliaji utekelezaji wa Programu hii, imeweza kutembelea sehemu zifuatazo ili kufahamu changamoto na mafanikio na kuweza kuishauri:

## A. SKULI YA SEKONDARI YA UFUNDI

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SKULI YA SEKONDARI YA UFUNDI MIKUNGUNI**

*(a)* Uchakavu wa majengo ya skuli na hali ya mazingira isiyoridhisha

*(b)* Uhaba na uchakavu wa Mashine katika Idara ya 'Mechanics' ambazo zimeonekana kuharibika mara kwa mara.

*(c)* Ukosefu wa Dakhalia ya wanafunzi wa kiume, hali inayosababisha wanafunzi kuishi katika mazingira magumu ya kimasomo.

*(d)* Ukosefu wa usafiri kwa wanafunzi, hali inayopelekea kuzorota kwa utekelezaji wa majukumu wakati wanafunzi wanapohitaji kwenda kufanya mafunzo ya kujifunza katika Taasisi tofauti za Serikali.

*(e)* Uhaba wa watendaji hali inayokwaza utekelezaji wa kazi za skuli kwa ufanisi, ambapo walimu wengi wa Kiwanda cha Ufundi Seremala na Sehemu ya Ufundi wa 'Welding' wamestaafu.

*(f)* Uzio wa Skuli haujakamilika, hali hiyo inasababisha wahalifu kuweza kuingia katika maeneo ya Skuli hiyo na kufanya matukio ya uhalifu pamoja masuala ya udhalilishaji.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

***(a)*** Kamati inaishauri wizara kusimamia utekelezaji wa mpango wa kuzifanyia ukarabati kwa ajili ya kuziimarisha Skuli za Ufundi ya Mikunguni Unguja na ile ya Kengeja Pemba,skuli ambazo zinahistoria kubwa katika maendeleo ya elimu Zanzibar**.**

***(b)*** Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kulitafutia ufumbuzi suala la ukosefu wa baadhi ya mashine muhimu za kufundishia mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi wa Skuli ya Sekondari ya Ufundi Mikunguni kwa ajili ya kuweza kupata ujuzi na taaluma ya ufundi, ili wanafunzi hao wanapomaliza masomo yao

waweze kuendelea na vyuo vyengine kwa masomo na hatimae kujiajiri wenyewe au kuajiriwa.

***(c)*** Kamati inapendekeza kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na Skuli ya Sekondari ya Ufundi Mikunguni kuanzisha Dakhalia ya wanafunzi wa kiume kwani hivi sasa ipo Dakhalia ya wanafunzi wanawake na Dakhalia ya wanafunzi wa kiume ipo ila hairidhishi, hali ambayo inapelekea baadhi ya wanafunzi wanaume kuishi katika mazingira magumu.

***(d)*** Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuipatia Skuli ya Sekondari ya Ufundi Mikunguni usafiri wa kudumu kwa ajili ya wanafunzi ili waweze kuondokana na changamoto hiyo hasa pale wanapopangiwa kufanya mafunzo ya vitendo katika taasisi nyengine zilizopo nje ya maeneo ya skuli.

***(e)*** Kamati inapendekeza kwa Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora wakati inapotangaza nafasi za ajira ni vyema kuzingatia uajiri wa wataalamu wenye fani na taaluma zinazohitajika katika Skuli ya Sekondari ya Ufundi Mikunguni ili kuondoa kadhia ya ukosefu wa wataalamu wa masomo mbali mbali katika Skuli hiyo.

***(f)*** Kamati inaendelea kuishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na Skuli ya Sekondari ya Ufundi Mikunguni kuukamilisha ujenzi wa uzio wa Skuli hiyo kwa lengo la kuzuia wahalifu wasiingie ndani ya eneo hilo la skuli pamoja na kuwajengea wanafunzi wetu kuishi katika mazingira mazuri na yaliosalama kwao.

***(g)*** Kamati inaipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia kwa kuweka utaratibu maalum kwa wanafunzi wanatoka Skuli ya Sekondari ya Ufundi Mikunguni kuweza kuendelea na masomo yao katika Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia (KITS) kwa kuwapunguzia gharama za malipo

ya masomo ili nao waweze kutimiza ndoto zao za kuendelea na masomo yao ya sayansi, kwani hivi sasa Zanzibar ina uhaba wa wataalamu wa masuala ya ufundi.

### B. CHUO CHA KIISLAMU UNGUJA

Chuo cha Kiislamu kina majukumu ya kutoa mafunzo ya ualimu kwa walimu watarajiwa (Pre - Service) kwa ngazi ya cheti na stashahada za msingi na sekondari kwa masomo ya Sayansi, Dini/Kiarabu na Sanaa kwa ujumla. Mafunzo hayo yanatolewa kwa lengo la kupata walimu mahiri na wenye uwezo wa kutoa taaluma sahihi kwa wanafunzi.

**CHANGAMOTO ZINAZOZIKABILI CHUO CHA KIISLAMU UNGUJA**

*(a)* Kumekuwa na idadi ndogo ya wanafunzi wanojiunga katika mafunzo ya ualimu kwa upande wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Diploma ya Dini na Kiarabu.

*(b)* Kukosekana kwa mazingira bora ya kujifunzia kutokana na upungufu wa vifaa vyakufundishia na kujifunzia hasa katika maabara za masomo ya Sayansi, TEHAMA na Maktaba.

*(c)* Kutokupatikana kwa huduma ya maji ya uhakika katika chuo cha kiislam

*(d)* Kutokuwa na gari wa kubebea wangajwa hasa inapotokea dharura wakati wa siku

*(e)* Uchakavu wa majengo pamoja na dakhalia hasa dakhalia wa wanafunzi wa kiume miundombinu yake mibofu hasa ya vyooni.

*(f)* Uchache wa madarasa unaopelekea kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi kwenye daraza moja.

*(g)* Eneo la chuo cha kiislam lina mgogooro na wamiliki wa mali

*(h)* Upungufu wa wafanyakazi kama vile walinzi, mtunza maabara, wakutubi, mshika fedha, wahudumu, katibu mukhtasi.

## MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

***(a)*** Kamati inashauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kuandaa utaratibu wa upatikanaji wa wataalamu wa huduma za afya katika Dakhalia za vyuo. Kwani Kamati imebaini kuwa wanafunzi wanaoishi ndani ya Chuo wanakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo za ukosefu wa wataalamu wa afya pale inapotokezea mwanafunzi kupata tatizo la kiafya wakati wa usiku na kukosekana kwa huduma hizo katika mazingira ya Chuo.

***(b)*** Kamati inapendekeza kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na Uongozi wa Chuo kulitafutia ufumbuzi wa kudumu suala la ukosefu wa usafiri wa uhakika kwa walimu pamoja na wanafunzi ili kuweza kuondokana na changamoto ya walimu kuchelewa kuanza kwa vipindi vya masomo pamoja na kupunguza uchelewaji wa wanafunzi madarasani.

***(c)*** Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kufanya marekebisho ya Mtaala wa Vyuo vya Ualimu vilivyopo nchini ili kuweza kwenda sambamba na mahitaji ya mabadiliko ya mifumo ya elimu nchini.

***(d)*** Kamati inaendelea kupendekeza kwa Serikali kuwepo kwa posho la mazingira magumu kwa walimu wote wanaosomesha katika maeneo ambayo hakuna usafiri wa uhakika.

***(e)*** Kamati inaishauri Serikali kuandaa mpango Mkakati wa uhamasishaji wa wanafunzi kujiunga na mafunzo ya ualimu kwa upande wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Diploma ya Dini na Kiarabu ili kupunguza uhaba wa walimu wa kada hizo katika Vyuo vyetu.

***(f)*** Kamati inaiomba Serikali kutenga bajeti maalum kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika maabara zetu za masomo ya sayansi, TEHAMA pamoja na maktaba.

*(g)* Kamati inaishauri Serikali kulitafutia ufumbuzi wa haraka suala la uvujaji wa madarasa pamoja na majengo ya dakhalia wanayoishi wanafunzi, hali inayopelekea kutokuwepo kwa mazingira rafiki ya kujifunzia na kufundishia.

*(h)* Kamati inaishauri Wizara kulitafutia ufumbuzi eneo lenye mgogoro kwenye eneo la chuo hicho.

*(i)* Kamati inaishauri wizara kuwachimbia kisima chuo cha kiislam ili kuondokana na changamoto ya kutokuwa na huduma ya maji ya uhakika

*(j)* Kamati pia inaishauri wiazara kutafutia gari maalum chuo hicho ili kutumika pale inapotokea dharura hasa nyakati za usiku.

## 3. PROGRAMU YA UBORA WA ELIMU

Programu hii imeundwa na Programu Ndogo Moja ambayo inalenga kusimamia elimu bora katika ngazi zote za elimu na kutoa huduma za Kuandaa Mitaala na Kuratibu Uandaaji wa Vitabu na Vifaa vya Kujifunzia na Kufundishia, Kutayarisha na Kusimamia Mitihani, Ukaguzi katika ngazi ya Elimu ya Skuli na katika Mfumo wa Elimu, Kutoa Taaluma ya Habari na Mawasiliano, ili itumike kama nyenzo ya Kufundishia na Kujifunzia, Kusajili Skuli na Kutoa Leseni za Walimu, Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha, Kutoa fursa kwa jamii kujisomea na kutafuta taarifa za kielimu na kuibua vipaji vya michezo kwa wanafunzi.

Lengo kuu la kuwepo huduma hizi ni kuhakikisha kwamba elimu inayotolewa katika ngazi zote za elimu ni yenye ubora kwa manufaa ya wenye kuhitimu, jamii na Taifa kwa ujumla.

Jumla ya TZS 8,124,600,489/- zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii kwa kipindi cha Julai – Disemba, 2023 ambapo TZS 6,466,674,880/- zilipatikana sawa na asilimia 80.

Kamati katika ufuatiliaji wa Programu hii, imeweza kutembelea sehemu zifuatazo ili kufahamu changamoto na mafanikio na kuweza kuishauri Serikali

## A. TAASISI YA ELIMU

Taasisi ya Elimu Zanzibar (TEZ) ni wakala wa serikali chini ya Wizara ya elimu na mafunzo ya amali. Taasisi imeanzishwa kwa sheria nambari 4 ya mwaka 2016 na imepewa mamlaka ya kutaarisha mitaala na vifaa vya kufundishia katika skuli na vyuo vya ualimu vya serikali na binafsi. Vile vile Taasisi inajukumu la kudhibiti ubora wa mitaala, kufanya tafiti za kielimu pamoja na kutoa mafunzo kwa walimu na wakufunzi wa vyuo vya aualimu juu ya matumizi ya mitaala na vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

**CHANGAMOTO**

- Uhaba wa watumishi katika idara na vitengo vya taasisi
- Ukosefu wa ofisi ya kudumu na yenye nafasi unguja na Pemba jambo ambalo linapelekea kutumia fedha nyingi za serikali kwa ajili ya kulipaia kodi
- Kutokamilika kwa sheria ya taasisi ya elimu jambo ambalo linainyima taasisi haki ya kuweza kusimamia majukumu yake kiusahihi.
- Ufinyu wa Bajeti kwa taasisi inayopelekea taasisi kutokufikia malengo yake iliyojiwekea.

**MAONI /USHAURI WA KAMATI**

a) Kamati inaishauri Wizara ya Elimu kuwaombea kibali cha kuajiri kwa Taasisi ya Elimu Zanzibar ili kuondokana na changamoto ya uhaba wa wafanyakazi.

b) Kamati inaiyomba Serikali kuwapatia jengo la kudumu Taassi ya Elimu Zanzibar ili kuondosha gharama wanazozitumia kwa kulipa kodi.

c) Kamati inaishauri Wizara kuharakisha Utungaji wa sheria ya taasis ya Elimu Zanzibar ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi

d) Kamati inaishauri wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na wizara ya fedha na mipango kuwaongezea bajeti Taasis ya Elimu Zanziabr ili kuweza kutekeleza majukumu yake vizuri.

e) Kamati inaishauri taasisi ya elimu kuunda tume ya walimu itakayoshughulikia nidhamu kwa walimu pamoja na ajira za walimu.
f) Kamati inashauri mitaala mipya izingatie teknologia ya tehama katika uimarishaji wa elimu.
g) Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara kukamilisha mchakato wa uchapishaji wa vitabu vya kufundishia kwa mujibu mtaala mpya wa elimu sambamba na mafunzokwa walimu yanahitaji kuendelezwa ili yaende sambamba na matumizi ya mtaala mpya.

## B. OFISI YA MKAGUZI MKUU WA ELIMU ZANZIBAR

Ofisi ya Mkaguzi wa Elimu (OICE) ni Wakala wa Serikali ulioanzishwa chini ya Sheria Nam. 10 ya mwaka 2018. Aidha, Ofisi inasimamiwa na Bodi ya Ushauri ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu iliyoundwa chini ya kifungu cha 10 cha Sheria ya kuanzishwa kwa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu. Jukumu kuu la Ofisi hii ni kusimamia ubora wa elimu nchini.

Vile vile, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu katika kusimamia Ubora wa Elimu hufanya ukaguzi wa elimu kwa skuli zote za Maandalizi, Msingi na Sekondari zilizosajiliwa pamoja na Taasisi zinazotoa Mafunzo ya Ualimu, Vyuo vya Elimu Mbadala, Elimu ya Watu Wazima, Taasisi za Elimu zilizosajiliwa zilizo nje ya Mfumo Rasmi wa Elimu.

## CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI OFISI YA MKAGUZI MKUU WA ELIMU ZANZIBAR

*(a)* Uchakavu na ufinyu wa nafasi katika jengo la mkaguzi Mkuu wa Elimu.
*(b)* Ukosefu wa Majengo ya Ofisi za wakaguzi wa mikoa, hali inayopelekea wakaguzi wa elimu kufanyakazi katika mazingira tofauti.
*(c)* Uhaba wa usafiri wa uhakika kwa Ofisi ya Mkaguzi wa Elimu, hali hiyo inapelekea kuzorota utekelezaji wa majukumu kwa Ofisi hiyo na

kushindwa kufikia malengo iliyojipangia wakati, ambapo kwa muda mwengine wakaguzi hutumia usafiri binafsi na wa kawaida na wakati mwengine huazima gari za Wizara kwa ajili ya kuweza kusaidia kutekeleza majukumu yao

*(d)* Stahiki za wakaguzi wa elimu; kukosa kutambuliwa katika miundo ya utumishi bado wakaguzi wamebaki katika kada ya walimu.

*(e)* Upungufu wa watendaji ambapo kuna haja ya upatikanaji wa watendaji ili kukidhi mahitaji ya muundo mpya wa Ofisi.

*(f)* Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu katika kufanya kazi zake za ukaguzi haiendani na Muongozo wa Ufikiwaji wa Miundombinu Rafiki kwa Watu Wenye Ulemavu katika skuli zetu zinazosomesha Elimu Mjumuisho katika ngazi ya Elimu ya Maandalizi, Msingi na Sekondari.

*(g)* Upungufu mkubwa wa wakaguzi wa masomo mapya kwa mujibu wa mfumo mpya wa mitaala.

*(h)* Kuwepo kwa OC ndogo kwa matumizi ya ofisi ni asilimia 30 ya matumizi.

*(i)* Upatikanaji wa taarifa za ukaguzi kwa baadhi ya skuli

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

***(a)*** Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuwatengea bajeti maalum kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu pamoja na Ofisi za Wakaguzi wa Elimu Mikoa ili kuweza kufikia malengo ya kuanzishwa kwa ofisi hizo kila mikoa kwa Unguja na Pemba.

***(b)*** Kamati inapendekeza kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu Zanzibar katika bajeti ya mwaka 2024/2025, suala la upatikanaji wa usafiri wa kudumu kwa Ofisi hiyo kupewa kipaumbele kwani kubaki kama ilivyo sasa inapelekea wakaguzi kupata ugumu wa kusimamia ubora wa elimu katika skuli zetu.

***(c)*** Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora zinapotangazwa nafasi za ajira mpya

kwa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu kuweza kuzingatia mahitaji ya kada zinazohitajika kwa ajili ya kufikia azma ya Serikali ya kukuza elimu nchini.

***(d)*** Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuliandalia utaratibu mzuri suala la ukaguzi wa elimu katika skuli zetu za Elimu Mjumuisho kuanzia ngazi ya Elimu ya Maandalizi, Msingi na hata Sekondari ili nao waende sambamba na mabadiliko ya Sekta ya Elimu Zanzibar.

***(e)*** Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kuwa kiwango cha ukaguzi kinaendana na wingi wa skuli yaani kiwango cha ukaguzi ni kidogo ikilinganisha na skuli nyingi zilizopo

***(f)*** Kmati inaishauri Wizara kuharakisha kuunda Baraza la Elimu ili kutoa nguvu za kisheria katika kutoa maamuzi dhidi ya makosa katika sekta ya elimu.

***(g)*** Kamati inaishauri Wizara kufuatilia upatikanaji wa nyongeza ya posho la walimu wakuu ambayo imepitishwa na Baraza la WAWAKILISHI katika bajeti ya wizara ili walimu hao waweze kupata stahiki zao.

## C. BODI YA HUDUMA ZA MAKTABA ZANZIBAR

Bodi ya Huduma za Maktaba Zanzibar ilianzishwa chini ya Sheria Namb. 7 ya mwaka 1993. Bodi ya Huduma za Maktaba inalenga zaidi kutoa huduma bora za Maktaba kwa jamii nzima ili kusaidia juhudi za Serikali katika kuinua kiwango cha elimu pamoja na kuleta maendeleo katika nyanja zote za maisha kwa kuweka misingi imara ya upatikanaji wa elimu na taarifa kwa umma.

Majukumu ya Bodi ya Huduma za Maktaba kwa mujibu wa kifungu cha 17(1) cha Sheria ya Bodi ya Huduma za Maktaba ya mwaka 1993, Bodi ni pamoja na :

*(a)* Kuanzisha, kukuza na kuendeleza Huduma za Maktaba katika Visiwa vya Zanzibar;

(b) Kuhakikisha upatikanaji wa vitabu na machapisho mengineyo kutoka kwa waandishi mbali mbali wa ndani na nje ya Zanzibar;

(c) Kuanzisha, kusimamia na kuendeleza Maktaba za Umma katika ngazi za Mikoa na Wilaya

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI BODI YA HUDUMA ZA MAKTABA.**

(a) Uhaba wa wataalamu hasa wakutubi na maafisa waendeshaji katika Maktaba zetu za Unguja na Pemba.

(b) Tatizo la usafiri kwani Ofisi ina gari mbili moja Unguja na moja Pemba na haziko kwenye hali nzuri hivyo kushindwa kufuatilia na kutekeleza majukumu yao ya Ofisi kwa ufanisi mzuri.

(c) Uwepo wa miundombinu chakavu ya jengo na uhaba wa nafasi.

(d) Tatizo la uhaba wa vitendeakazi hasa vifaa vya TEHAMA na vifaa vya kuendeshea programu za maktaba hususan watu wenye ulemavu na watoto.

(e) Uchache wa vitabu ndani ya maktaba hali inayopelekea wanafunzi kushindwa kupata baadhi ya vitabu kwenye maktaba ambazo ziko karibu na maeneo yao na kupelekea kuvifuata masafa marefu na wakati mwengine kuvikosa kabisa.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inashauri Serikali kulipatia ufumbuzi suala la uchache wa wataalamu katika Bodi ya Huduma za Maktaba kwa kutoa kibali cha uajiri ili huduma zitolewe kwa ufanisi zaidi.

(b) Kamati inapendekeza kwa Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuandaa mpango Madhubuti wa ununuzi wa vifaa kwa Bodi ya Huduma za Maktaba pamoja na kuwawekea miundombinu rafiki wanafunzi pamoja na watu wenye ulemavu ili waweze kunufaika na huduma zinazotolewa na Maktaba hizo.

*(c)* Kamati inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na Bodi ya Huduma za Maktaba kuifanyia marekebisho Sheria Nam. 7 mwaka 1993 ya Bodi ya Huduma za Maktaba, kwani Sheria hiyo imekuwa na mapungufu mengi na haina Kanuni ya kusaidia utekelezaji wa Sheria hiyo.

*(d)* Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuiongezea bajeti Bodi ya Huduma za Maktaba, kwa ajili ya kuweza kutekeleza majukumu yake iliyojipangia kwa ufanisi.

*(e)* Kamati inaishauri Bodi ya Huduma za Maktaba kutenga Bajeti Mahususi kwa ajili ya ununuzi wa gari ya Ofisi.

### (D) BARAZA LA MITIHANI

Baraza la mitihani Zanzibar limeanzishwa kwa sheria nambari sita ya mwaka 2012 ambapo jukumu lake la msingi ni kufanya upimaji kwa wanafunzi ili kujua kiwango cha maarifa, umahiri na mwelekeo waliopata baada ya kujifunza.

### CHANGAMOTO ZINAZOZIKABILI BARAZA LA MITIHANI ZANZIBAR

- Uhaba wa nafasi katika jengo la ofisi.
- Kukosekana kwa mtambo wa kisasa kwa ajili ya uchapaji wa mitihani hali ambayo Baraza hulazimika kuchapisha mitihani katika kiwanda cha Wakala wa Serikali wa uchapaji jambo ambalo linaweza kutokuwa na usiri wa mitihani pamoja na kutumia fedha nyingi za kuchapisha.
- Baraza kutomiliki majengo kwa ajili ya vituo vya mitihani. Hali hii huleta usumbufu mkubwa katika zoezi la usahihishaji wa mitihani

### MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

- Kamati inaipongeza Wizara kupitia Baraza la Mitihani kwa kusimamia ufanyaji, usahihishaji na Kutoa Matokeo mazuri ya Mitihani ya Darasa la

Nne yenye asilimia ya ufaulu 91.35 na aslimia 95.00 kwa ufaulu wa darasa la Saba.

- Kamati inaishauri wizara kuzingatia kupatikana kwa mtambo wa kisasa wa uchapishaji wa mitihani ili baraza liweze kujitegemea kufanya shughuli zake wenyewe na kuepuka gharama zisizo na msingi.
- Kamati inaishauri serikali kuwapatia jingo la ofisi baraza la mitihani kwani jingo ambalo wanalotumia sasa ni chakavu na haliwatoshi kutokana na majukumu yao.
- Kamati inalishauri Baraza la Mitihani Zanzibar kuandaa rasimu ya marekebisho ya Kanuni za Baraza la Mitihani Zanzibar.

## 4. PROGRAMU KUU YA ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI

Programu hii ina lengo la kutoa elimu ya mafunzo ya amali kwa mwanafunzi kulingana na mahitaji ya soko la ajira, kupunguza idadi ya wasiojua kusoma na kuandika na kuwawezesha vijana kitaaluma ili waweze kujiajiri na kuajirika.
Jumla ya TZS 18,109,178,450/- zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii ambapo TZS 5,327,211,229/- sawa na asilimia 29 zilipatikana.

### CHANGAMOTO

- Upungufu wa wakufunzi wenye sifa zinazohitaajika katika ufundishaji katika Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Mkokotoni
- Uhaba wa fedha katika kufanya utafiti mbali mbali kuhusiana na mafunzo ya amali.
- Ukosefu wa vitendea kazi kwa ajili ya usimamizi na uendeshaji wa mifumo kama e-office, e-procurement, HR PayRole.

### MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

- Kamati inaishauri Mamlaka ya mafunzo ya amali kujitangaza kibiashara ili iweze kutekelza lengo lililokusudiwa

- Kamati inaishauri Wizara kuvizingatia vyuo vya mafunzo ya mali kuwa na muundo maalumu tofauti na taasisi nyengine ili kuwawezesha watendaji wanaostahiki kupata haki zao kwa mujibu wa muundo wa vyuo.
- Kamati inaishauri Wizara kuimarisha mitaala ya vyuo vya amali ili wataalamu wanaotolewa katika vyuo hivyo waweze kufikia vigezo vinavyohitajika katika soko la ajira hasa soko la utalii wa mahoteli.
- Kamati inaishauri Wizara kufanya tathmini ili kufahamu muitiko wa maendeleo ya vyuo vyengine vya mafunzo ya amali vilivyopo nchini
- Kamati inaishauri Wizara kuipatia Mamlaka ya Mafunzo ya amali mchango wa kodi ya kuendeleza ujuzi ya SDL inayotolewa na wawekezaji wa mahoteli ili iweze kuimarisha vyuo hivyo.

## 5. PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Programu hii ina lengo la kuhakikisha nyenzo zilizo bora zinapatikana na zinatumika kwa kuimarisha utoaji na upatikanaji wa elimu. Programu hii ina programu ndogo tatu zikiwemo program ndogo ya Ungozi kwa Jumla, program ndogo ya Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti na program ndogo ya Uratibu wa shughuli za Elimu Pemba.

Katika mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya Tanzania shilingi 26,578,870,277/= zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha programuu hii.

Kwa kipindi cha Julai -Disemba, 2023 programu hii ilipangiwa jumla ya TZS. 12,756,470,933/-. Hadi kufikia Disemba 2023, jumla ya TZS. 10,186,813,161/- sawa na asilimia 80 zilipatikana.

## CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

*(a)* Kuwepo kwa ongezeko kubwa la fedha katika ujenzi wa miradi yote inayotekelezwa kupitia fedha za UVIKO 19 hali iliyopelekea Wizara

kuongeza fedha za ziada (variations) ili kufanikisha ujenzi wa miradi hiyo.

*(b)* Uhaba wa fedha za Mikopo kwa wanafunzi waliojiunga na Elimu ya Juu hasa wanaosoma nje hali inayowapelekea baadhi ya wakati kuzuiwa kufanya mitihani yao au kusimamishwa kuendelea na masomo.

*(c)* Uhaba wa walimu wa Sayansi katika skuli zote za Unguja na Pemba. Mfano halisi, Skuli ya Mkwajuni kwa mwaka huu Wizara imeanzisha darasa la michipuo ila walimu wa Sayansi katika Skuli hiyo hakuna.

*(d)* Kuwepo kwa ongezeko kubwa la idadi ya walimu wasiothibitishwa kwa kupatiwa leseni za kufundisha.

*(e)* Kutokuwepo kwa vitabu vya mitaala katika skuli za Serikali hali inayopelekea ufaulu mdogo wa wanafunzi hususan kwa wanafunzi wa sayansi.

*(f)* Kutokuwepo kwa maeneo maalum ya kusahihishia mitihani hali inayopelekea Baraza la Mitihani kukodi maeneo ya watu binafsi kwa fedha nyingi na yasio salama kwa ajili ya kusahihishia mitahani kinyume na matakwa ya Sheria ya Kuanzisha Baraza hilo.

*(g)* Kuchelewa kupatikana kwa vibali vya ajira kwa nafasi za ajira mpya hali inayosababisha uhaba wa walimu katika maeneo yote ya Unguja na Pemba.

*(h)* Kupanga kwa makadirio makubwa ya Mapato ya Wizara kinyume na hali halisi ya makusanyo ya Mapato hayo.

*(i)* Kutokuwepo kwa usafiri wa uhakika kwa wakaguzi wakati wanapokwenda kufanya ukaguzi katika Skuli za Maandalizi, Msingi na Sekondari hasa katika skuli zilizopo kwenye visiwa.

*(j)* Posho dogo kwa wakaguzi wetu wa ndani wanaokwenda kufanya ukaguzi katika skuli zilizopo kwenye visiwa kama vile Fundo, Kokota,

Kojani, Tumbatu, hali inayowasababishia kukaa dago kwa ajili ya kutekeleza shughuli zao za ukaguzi.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inaishari Wizara kuhakikisha inatekelezwa ipasavyo Miradi ya Kuimarisha elimu ya juu kwa mageuzi ya kiuchumi (HEET)na mradi wa kuimarisha ujuzi kwa vijana katika kujipatia ajira katika Uchumi wa Buluu (SEBEP).

(b) Kamati inaishauri Serikali kuunda Kamati Maalum ya kitaalam Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mikataba inayoingiwa baina ya Serikali na Wakandarasi mbali mbali kwa lengo la kujenga usimamizi imara na kujiridhisha kwa thamani ya fedha inalingana na ubora wa utekelezaji wa miradi tuliokubaliana madhubuti.

(c) Kamati inaishauri Wizara inapotekeleza Miradi ya Maendeleo katika Sekta yoyote lazima kuwashirikisha kikamilifu watendaji wa Taasisi husika na uhitaji uendane na utekelezaji wa mradi husika. ili kuepusha changamoto ya upotevu wa fedha za Serikali.

(d) Kamati pia inaishauri Serikali kwa Kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuipunguza mzigo Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ya Wizara kushughulikia na kusimamia miradi yote ujenzi kwa kurudisha Idara ya Ujenzi kama ilivyo kuwa awali kwa lengo la kupunguza changamoto zinazojitokeza za matumizi makubwa ya fedha za ziada (variations) kinyume na utaratibu uliopo kisheria.

(e) Kamati inashauri Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu kusomesha wanafunzi katika vyuo vyetu vya ndani hasa kwa “Course” zinazopatikana ndani badala ya kutumia fedha nyingi za kugharamia wanafunzi kwenda vyuo vya nje na kutilia mkazo fani zinazoendana na vipaombele vya Taifa na Sera ya Uchumi wa Buluu.

(f) Kamati inaishauri Serikali pamoja na Wizara kabla ya kuanza kwa ujenzi wa miradi yoyote kufanyike upembuzi yakinifu wa maeneo yanayokwenda kujengwa mradi kabda ya kuanza kwa ujenzi ili kuipunguzia Serikali matumizi ya ziada.

(g) Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuwapatia mafunzo kila baada ya muda wahandisi wetu wa ndani wa Wizara pamoja na Watu wa Manunuzi kwani Kamati imegundua kuwa ongezeko lililojitokeza katika miradi hii mikubwa ya ujenzi wa skuli umechangiwa kwa kiasi kikubwa na wasimamizi wetu kutokuwa na utaalamu wa kutosha katika masuala ya usimamizi wa miradi mikubwa na mingi kwa wakati mmoja.

(h) Kamati inaishauri wizara kupitia taasisi ya karume ya sayansi na Technologia (KIST) kuwa wabunifu katika kuishauri serikali kuhusu masuala ya mafuta na gesi badala ya kutumia wataalamu wa fani hizo kutoka nje. Sambamba na kuipongeza Taasisi ya Karume kwa nia yake ya kuanzisha Tawi jipya Pemba.

(i) Kamati pia inaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa juhudi kubwa walizochukua katika kufanya ukarabati na ujenzi wa Madarasa na Majengo ya Ghorofa ya Skuli za kisasa kwa Unguja na Pemba katika kuhakikisha wanafunzi wanasoma katika mazingira rafiki na salama.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 WIZARA YA AFYA

Wizara ya Afya (Fungu H01) inaundwa na Idara tano (5), Taasisi (5), Mabaraza Matano (5), na Bodi kama ifuatavyo:

**IDARA**

*(i)* Idara ya Uendeshaji na Utumishi;

*(ii)* Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;

*(iii)* Idara ya Kinga na Elimu ya Afya;

*(iv)* Idara ya Mfamasia Mkuu wa Serikali;

*(v)* Idara ya Bohari Kuu ya Dawa; na

**TAASISI**

*(i)* Hospitali ya Mnazi Mmoja;

*(ii)* Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi;

*(iii)* Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali;

*(iv)* Maabara ya Afya ya Jamii - Pemba; na

*(v)* Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar.

**MABARAZA YA KITAALUMA/BODI**

*(i)* Baraza la Wauguzi na Wakunga;

*(ii)* Baraza la Madaktari;

*(iii)* Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala;

*(iv)* Baraza la Afya ya Jamii;

*(v)* Baraza la Wataalamu wa Afya ya Mazingira;

*(vi)* Baraza la Wataalamu wa Maabara za Afya; na

*(vii)* Bodi ya Ushauri wa Huduma za Hospitali Binafsi.

Kamati katika utekelezaji wa kazi zake kwa mwaka wa fedha 2023/2024, ilifatilia utekelezaji wa Bajeti inayotumia Programmu ambapo Wizara ya Afya ilipanga kutekeleza programu zifuatazo:

*(i)* Programu Kuu ya Kinga na Elimu ya Afya;

*(ii)* Programu Kuu ya Huduma za Tiba;

*(iii)* Programu Kuu ya Uratibu na Uendeshaji wa Wizara ya Afya; na

*(iv)* Programu Kuu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Wizara inatekeleza Programu hizo kupitia taasisi zake zilizoainishwa hapo juu. Katika kufuatilia utekelezaji wa Programu hizo, Kamati ilifanya ziara katika Hospitali na Taasisi mbali mbali kwa lengo la kuona mafanikio na changamoto zinazokwamisha utekelezaji wa Programu hizo ili kuishauri Serikali namna bora itakayoweza kutumika katika kuzipatia ufumbuzi wa kudumu changamoto hizo.

**1. PROGRAMU KUU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA(PHO1)**

Progaramu hii ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kinga na kuongeza uelewa wa jamii juu ya njia mbali mbali za kujikinga na maradhi yakiwemo ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza.

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya shilingi Bilioni Thelathini na Sita, Milioni Mia Nane na Tisini na nane laki tatu na sitini na nne elfu (36,898,364,000/=) sawa na asilimia 19.4 ya Bajet ya Wizara zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbali mbali za programu hii.

Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2023, Idara ya Kinga na Elimu ya Afya ilikadiriwa kuingiziwa jumla ya shillingi 11,104,639,798/= Kati ya fedha hizo shillingi 11,759,963,824.00/= zilingizwa kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 127.1. Ongezeko hili ni kutokana na wajiriwa wapya na malimbikizo ya stahiki zao baada ya mabadiliko ya mishahara yalioanza Julai 2023, aidha shillingi 195,000,000.00/= kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji sawa na asilimia 10.5.

Programu hii imeweza kutekeleza shughuli zake mbali mbali zikiwemo:

- Huduma za Kumaliza Malaria Zanzibar
- Huduma Shirikishi za Afya ya Uzazi na Mtoto
- uduma Shirikishi za UKIMWI, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma.

**A. ZIARA YA KAMATI KITUO CHA AFYA RAHALEO**

Katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa Programuu hii, Kamati ilifanya ziara

Katika Kituo cha Afya cha Rahaleo. Kituo hiki ni miongoni mwa vituo 10 kutoka Wilaya ya Mjini ambacho kina wafanyakazi 44. Kituo cha Rahaleo kinahudumia Shehia 7.

**CHANGAMOTO**

- Kuongezeka kwa idadi ya wagonjwa na kupelekea msongamano mkubwa katika upatikanaji wa huduma za afya.
- Upungufu wa vyumba vya huduma mbali mbali: Mfano Maabara
- Upungufu wa wafanyakazi; Madaktari, Wauguzi
- Kukosekana kwa mfumo uangamizaji taka

**USHAURI /MAONI YA KAMATI**

- Kamati inashauri Wizara katika Mpango wa kuviimarisha vituo 74 vya afya kuhakikisha kuwa wataalamu wa afya wanashirikishwa ipasavyo katika Miradi ya Ujenzi wa Vituo hivyo ili kuondokana na changamoto mbali mbali zinazoweza kujitiokeza wakati wa utoaji wa huduma.
- Kamati inaishauri Wizara kuharakisha kukamilisha taratibu za manunuzi ili Mpango wa ujenzi wa kuviimarisha vituo vya afya uweze kutekelezwa kwa wakati.
- Kamati inaishauri Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wizara ya HABARI, kufuatilia upatikanaji wa eneo lililohifadhiwa makontena ndani

ya eneo la ZBC Radio, ili liweze kuingizwa katika mpango wa utanuzi wa Kituo cha afya cha Rahaleo.

## 2. PROGRAMU KUU YA TIBA

Jukumu kuu la programu hii ni kusimamia utoaji wa huduma bora za afya kwa Hospitali za Wilaya na Mikoa pamoja na kusimamia Taasisi mbali mbali za Wizara zikiwemo Mpango wa Damu Salama, Hospitali Binafsi, Huduma za Uchunguzi, Baraza la Wauguzi na Wakunga, Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi, Bohari Kuu ya Dawa, Afisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Afisi ya Mfamasia Mkuu wa Serikali, Baraza la Madaktari na Taasisi ya Utafiti wa Afya.

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya shilingi Bilioni mia moja na kumi na saba, milioni arobaini na saba, laki tisa na arobaini na sita elfu (117,047,946,000/=) sawa na asilimia 61.8 zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbali mbali za programu hii kupitia  Programu ndogo ya Matibabu na Uchunguzi.

Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2023, Idara ya Tiba ilikadiriwa kuingiziwa jumla ya shillingi 28,770,229,032/= Kati ya fedha hizo shilling 9,361,917,706/= zilingizwa kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 151. Ongezeko hili ni kutokana na mbadiliko ya mishahara na wajiriwa wapya yalioanza Julai 2023, aidha shillingi 15,584,294,246.00/= kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji sawa na asilimia 69.1

Kamati iliweza kufuatilia utekelezaji wa Programu hii katika taasisi kama ifuatavyo:

### A. WAKALA WA BOHARI KUU YA DAWA ZANZIBAR

Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa ina jukumu la kupokea, kuhifadhi na kusambaza dawa, vifaa vya utabibu, kitendanishi pamoja na vifaa vyengine

vya uchunguzi kwenye hospitali na vituo vyote vya afya vya Serikali na baadhi ya vituo vya binafsi Unguja na Pemba.

## CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WAKALA WA BOHARI KUU YA DAWA

(a) Uhaba wa Rasilimali watu ikiwemo wafamasia, fundi sanifu dawa, afisa TEHAMA, afisa manunuzi, mkaguzi wa ndani, mafundi, wahasibu, ‘biomedical engineer’ na wanasheria.

(b) Bajeti ndogo ya kuendeshea huduma za usambazaji wa dawa kwa ufanisi.

kwa Wakala wa Bohari ya Dawa

(c) Uhaba wa vitendeakazi (Forklift na pallet stackers) na kompyuta.

(d) Uchache wa leseni za ‘mSupply’ jambo linalopelekea ucheleweshaji wa huduma za usambazaji unaotokana na msongamano wa watumiaji.

(e) Kukosekana kwa ulinzi wa uhakika katika Bohari Kuu ya Dawa Pemba.

(f) Uletaji wa dawa za misaada katika Wakala wa Bohari bila ya taarifa kwa wakati.

(g) Uhaba wa mawasiliano baina ya Bohari Kuu ya Dawa, Afisi ya Mfamasia Mkuu wa Serikali, Kitengo cha Manunuzi na Wahasibu hali ambayo inakosesha ufanisi kwenye mnyororo wa ugavi.

(h) Uhaba wa nafasi ya kuhifadhia dawa

(i) Upungufu wa wafanyakazi wa kada ya sheria, mhasibu, manunuzi masoko wakati taasisi hiyo tayari ipo katika Mfumo wa Wakala

(j) Ukosefu wa mfumo unaounganisha bohari na vituo vya afya hali inayopelekea kutopata taarifa za dawa zilizopo Bohari au vituoni

## MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

(a) Kamati inaishauri Wizara kuharakisha mpango wa mradi wa ujenzi wa jengo jipya la Bohari ya kisasa ili kuongeza nafasi ya kuhifadhia dawa na vifaa vya utibabu.

(b) Kamati inapongeza Wizara kwa kuweza kuibadilisha sharia ya bohari kuu kuwa wakala wa Bohari ya dawa zanzibar

(c) Kamati inaishauri Wakala wa Bohari kutanua wigo wa mfumo wa usambazaji wa dawa uliopo ili kurahisisha upataikanaji wa taarifa za dawa vituoni na Baohari.

(d) Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kuandaa utaratibu maalum kwa dawa zinazonunuliwa kwa ajili ya Hospitali na vituo vya Afya Pemba kupelekwa moja kwa moja Pemba ili kuepusha ucheleweshaji wa huduma kwa hospitali na vituo hivyo.

(e) Kamati inaishauri Serikali juu ya suala zima la upatikanaji wa leseni za 'mSupply' kuongezwa ili kwenda sambamba na mafunzo kwa wafanyakazi kuhusu matumizi ya mfumo huo kwa Unguja na Pemba ili kuongeza ufanisi katika kazi zao.

(f) Kamati inaishauri Wizara ya Afya kushirikiana na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ juu ya suala zima la kupatiwa walinzi katika maeneo yao ya Bohari ili kuimarisha usalama wa mali za Serikali.

(g) Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Afya kwamba misaada yote inayoletwa kutoka kwa Wahisani mbali mbali kwenda Bohari Kuu ya Dawa ifuate utaratibu uliopo chini ya Ofisi ya Mfamasia Mkuu wa Serikali ili kuepusha uingizwaji wa dawa zilizokuwa zimeshamaliza muda wa matumizi.

(h) Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuiongezea bajeti Bohari ya Kuu ya Dawa kwa lengo la kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi ili kuondokana na uchelewaji wa uangizaji wa dawa nchini.

(i) Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Taasisi ya Serikali Mtandao kurekebisha kasoro ndogo ndogo ambazo zinasababisha

kuzorota kwa suala la urahisishaji wa usambazaji wa dawa kupitia Mtandao.

(j) Kamati inaishauri Serikali kuandaa utaratibu wa kuipatia Bohari ya Dawa ya Vitongoji wafanyakazi wa kutosha pamoja na kuwajengea uwezo wafanyakazi ili waweze kufanya shughuli zao bila ya kutegemea watendaji kutoka Bohari Kuu ya Dawa Maruhubi.

## B. MFAMASIA MKUU WA SERIKALI

Ofisi ya Mfamasia mkuu wa serikali ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sera ya dawa (National Medicine Pilicy), ikiwa na pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa dawa muhimu na vifaa Tiba vya utibabu, pamoja na utumiaji sahihi wa dawa (Rational Medicine Use).

### 1. Kuratibu ununuzi wa dawa muhimu na vifaa vya utibabu

Katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2023-2024, jumla ya fedha shilingi Tzs 13,690,935,00/= zilipangwa kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba kwa hospitali za mkoa, wilaya na vituo vya afya kati ya hizo fedha zilizopatikana ni shilingi TZs 12,658,268,995/= sawa na asilimia 92.

Kati ya fedha hizo, shilingi 9,540,000,000/= zilitumika kwa ununuzi wa dawa za hospitali za Mkoa, Wilaya na vituo vya afya na malipo ya watoa huduma za uchunguzi.

Kwa upande wa Hospitali ya Mnazi Moja zimetumika jumla ya shilingi 5,460,000,000/- kwa kipindi cha Julai hadi Disemba kwa ununuzi wa dawa na vifaa tiba.

### 2. Uendeshaji wa kazi za Mfamasia Mkuu.

Katika uendeshaji wa kazi za Mfamasia Mkuu – (OC) jumla ya shilingi 163,849,166/= zilipangwa kati ya hizo shilingi 25,000,000 zilitumika sawa na asilimia 15%.

**CHANGAMOTO**

- Mgao mdogo wa OC na kucheleweshwa kutoka kwa hiyo OC hali inayoisababishia Ofisi kushindwa kutekeleza baadhi ya majukumu ambayo yamepangwa kutekelezwa kwa kipindi husika.
- Ukosefu wa Internent katika Vituo vya afya ambapo husababisha utumiaji wa mfumo na kukosa taarifa sahihi (data quality).
- Uchakavu wa gari za kufanyia ukaguzi katika Hospitali na Vituo vya afya na kupelekea kutofikia malengo yaliyopangwa.

**USHAURI/MAONI YA KAMATI**

- Kamati inaishauri Serikali kuiongezea mgao wa OC Ofisi ya Mfamasia Mkuu ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Asilimia 15 sawa na shilingi milioni 25 ya jumla ya OC ya zaidi ya shilingi Milioni 163 ndio iliyoweza kupatikana katika kipindi cha Julai hadi Disemba.
- Kamati inaishauri Wizara kuharakisha kazi ya uchapishwaji wa Muongozo wa matibabu (Standard Treatment Guidelines) wa mwaka 2014. Sambamba na Orodha ya dawa muhimu ya mwaka 2015 ili uweze kusambazwa na kutumika katika hospitali zote na vituo vya afya ndani ya nchi. Kamati imebaini kuwa kutokuwepo kwa muongozo huo kwa kipindi cha zaidi ya miaka 10 sasa kunahatarisha utoaji wa huduma za afya kwa jamii nchini.
- Kamati inaipongeza Wizara kupitia Mfamasia Mkuu, kwa kufanya mapitio ya dawa za uzazi wa mpango na dawa za kuokoa maisha kwa mama na mtoto ili kuweza kujua dawa zilizopo, zinazohitajika na zisizofaa katika kuimarisha huduma za upatikanaji wa dawa hizo na vifaa tiba.
- Kamati inaishauri Wizara kukamilisha zoezi la ukaguzi wa Hospitali na Vituo vya afya 31 vilivyobaki kati ya vituo 48 vilivyopangwa kukaguliwa katika Wilaya za Unguja sambamba na kuvifikia vituo kama hivyo kwa upande wa Pemba. Ofisi ya Mfamasia MKuu imeweza kuvikagua jumla ya

vituo 17 vya afya katika Wilaya ya Kati na Magharibi "B" vikiwemo Ukongoroni, Unguja Ukuu, Charawe na Marumbi.

- Kamati inapendekeza kwa Serikali kupitia Wakala wa Mkonga wa Mawasiliano (ZICTIA) kuimarisha huduma ya mtandao katika vituo vyote vya afya pamoja na hospitali kwa ajili ya kurahisisha utumaji wa taarifa muhimu za afya zikiwemo za matumizi na maombi ya dawa (R&R).
- Pamoja na jitihada za uimarishaji wa ongezeko la upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ulipaji wa madeni ya zamani ya dawa, Kamati inaishauri Wizara kupitia Mfamasia Mkuu wa Serikali kuhakikisha inakamilisha ulipaji wa madeni hayo ili Serikali iweze kuondoka na mzigo huo wa deni la dawa. Jumla ya shilingi 3,118,268,995/= zilitumika kwaajili ya ulipaji wa madeni ya zamani ya dawa na vifaa tiba.

## C. TAASISI YA UTAFITI WA AFYA ZANZIBAR (ZAHRI)

Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar (ZAHRI) imeanzishwa kwa Sheria Namba. 5 ya Mwaka 2018. Taasisi hii ni miongoni mwa Taasisi muhimu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa mujibu wa Sheria ya kuanzishwa kwake, Taasisi ya Utafiti wa Afya imepewa majukumu ya kusimamia upatikanaji wa taarifa za kisayansi kwa ajili ya kuendeleza na kuimarisha njia na mbinu mbali mbali za tiba na udhibiti wa magonjwa ya binaadamu nchini ili kufikia malengo yaliokusudiwa.

## CHANGAMOTO ZA TAASISI YA UTAFITI WA AFYA ZANZIBAR (ZAHRI)

(a) Taasisi hii inakabiliwa na changamoto mbali mbali kama vile fedha za kuendeshaa tafiti muhimu, fedha za kuendeleza ujenzi wa majengo yaliyokusudiwa kuwa maabara ya kuchunguzia wanyama, maabara ya 'Biochemistry'.

(b) Uhaba na usafiri wa uhakika kwa Taasisi.

(c) Kuchelewa kukamilishwa kwa muundo waUtumishi wa Taasisi.

(d) Kukamilisha uuandaaji wa Kanuni za fedha na Sera ya Taasisi

(e) Changamoto ya matumizi ya Mfumo wa Manunuzi ulioanzishwa na Mamlaka ya Manunuzi ya Serikali (e-proz), hali inayopelekea watumishi kushindwa kufanya malipo ya manunuzi yoyote ya Serikali.

(f) Ukosefu wa maeneo kwa ajili ya kuanzisha shamba darasa la mimea ya tiba asili ambayo inahitajika kufanyiwa utafiti kwa ajili ya matumizi ya binaadamu licha ya maombi ya kuwasilishwa kwenye Wizara husika na Kilimo.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inaishauri Wizara ya Afya kuhakikisha kuwa Taasi ya ZAHRI inakamilisha Muundo wake wa utumishi ili haki pamoja stahiki ya wafanyakazi ziweze kupatikana ipasavyo.

(b) Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuwapatia fedha Taasisi ya Utafiti wa Afya kwa ajili ya kukamilisha utekelezaji wa shughuli mbali mbali za Taasisi, asilimia ya fedha zinazoingizwa haifiki hata nusu ya malengo ya Ofisi.

(c) Kamati inaishauri Serikali kuipatia usafiri wa uhakika Taasisi hii ili kuwasaidia watendaji pamoja na Mkurugenzi Mkuu kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi hasa ikizingatiwa Taasisi yao iko nje ya Mji.

(d) Kamati pia inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuipatia eneo maalum Taasisi hii kwa ajili ya kuanzisha Shamba Darasa la mimea ya tiba asili kwa ajili ya kuenzi mimea adimu inayotoweka duniani ambayo ni muhimu kwa tiba ya afya kwa binaadamu.

(e) Kamati inaishauri Mamlaka ya Manunuzi Serikalini kabla ya kuanzisha mfumo wowote kuwapatia mafunzo watendaji wote wanaohusika na matumizi ya mfumo huo kwa lengo la kupunguza changamoto za matumizi yake.

## (D) WAKALA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI

Maaabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Zanzibar imegawika katika Idara kuu Sita ambazo ni zinazoendesha na kutekeleza shghuli zote za Taasisi.Idara zenyewe ni Idara ya Utawala na uendeshaji, Idara ya kemikali na mazingira, Idara ya chakula na dawa, Idara ya Sayansi ya makosa ya jinai, Idara ya Udhibiti Ubora wa Viwango pamoja na Idara ya Mratibu Pemba.

**CHANGAMOTO**

Kuchelewa upatikanaji wa baadhi ya vifaa vya maabara kutokana na utaratibu wa manunuzi ambapo hali hiyo hupelekea kazi za uchunguzi wa sampuli za kemikali na mazingira kuchelewa kufanyika.

- Maabara ya microbiologia kushambuliwa na tatizo la unyevu ambapo hali hiyo inapelekea kuleta uharibifu wa maabara hiyo.
- Ukosefu wa AC katika chumba cha kuhifadhia media pamoja na sampuli ambazo zinahitaji temperature maalum
- Kuwepo kwa uhaba wa wakaguzi wa kemikali ambapo hupelekea kutoimarika kwa ukaguzi katika maeneo ya bandari kama Mkokotoni, Kizimkazi pamoja na maeneo ya viwanja vya ndege.

**USHAURI/MAONI YA KAMATI**

- Kamati inapongeza kuongezeka kwa idadi ya wadau waliosajiliwa juu ya suala la udhibiti na usimamizi wa kemikali Zanzibar.
- Kamati inapongeza hatua ya kufanyiwa ukaguzi maeneo yote ambayo yamesajiliwa lakini hayakufanyiwa ukaguzi
- Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kuwa inawapatia wakaguzi wa kemikali wakala wa maabara ya mkemia mkuu wa serikali ili ukaguzi uweze kuimarika katika maeneo bandari na viwanja vya ndege.
- Kamati inashauri Wizara kuziopitia taratibu za manunuzi ili kurahisisha upatikanaji wa baadhi ya vifaa vya maabara na kazi za uchunguzi wa sampuli za kemikali na mazingira kuweza kufanyika .

- Kamati inashauri Wizara kuifanyia matengenezo Maabara ya microbiologia baada ya kushambuliwa na tatizo la unyevu ili maabara hiyo iweze kufanya kazi ipasavyo.

**(E) WAKALA WA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI**

Wakala wa Chakula, Dawa Na Vipodozi Zanzibar ina jukumu la kuimarisha na kudhibiti ubora na usalama wa Chakula, Dawa, Vipodozi na vifaa vya utibabu chini ya sheria nambari 3 ya mwaka 2017.

**CHANGAMOTO:**

- Wajasiri amali kukosa elimu ya kutosha na maelekezo ya kitaalamu ya uwekaji wa dawa hasa za kemikali katika vyakula na mazao ya kilimo ya biashara.
- Kukosekana kwa ofisi ya kudumu ya Wakala kisiwani Pemba jambo ambalo linachelewesha katika uimarishaji wa huduma za Wakala kisiwani humo.
- Uhaba wa wafanyakazi hususan katika sehemu za machinjio

**USHAURI /MAONI YA KAMATI**

- Kamati inapongeza ZFDA kwa utekelezaji wa majukumu yao kwa ufanisi.
- Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kuwa jengo jipya la Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodizi pamoja na vifaa vya uchunguzi vilivyowekwa katika jengo hilo kuwa linatuzwa ili kuwa na taasisi ya kitaalamu imara na yenye ubora. Mradi wa Jengo jipya la Maabara ya kisasa ya Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi ni mradi wa Maendeleo wa SMZ uliogharimu jumala ya shilingi za kitanzania bilioni 5.4 na awamu ya pili ni ununuzi wa vifaa vya maabara ambao umeharimu jumla ya shilingi za kitanzania Bilioni 4.4.
- Kamati imeishauri Wizara kuanzisha kituo cha pamoja ONE STOP CENTER katika maeneo ya uingiaji wa bidhaa kama bandari ili kudhibiti uingiaji wa bidhaa haramu za dawa na chakula pamoja na kurahisisha

usimamizi wa mfumo wa biashara wa bidhaa hizo wa pamoja ambazo zinaingia kutoka nchi na maeneo tofauti.

- Kamati inaishauri Wizara kuangalia namna bora ya kuweza kuimarisha Maabara ya Wakala Pemba ili kunusuru afya za wananchi kutumia dawa pamoja na chakula salama ambavyo vinapata ithibati ya uhalali wa matumizi yake kutoka kwa chombo hicho cha kitaalamu.
- Kamati inaishauri Wizara kuharakisha kulitumia eneo la Wakala (ZFDA) lililopo Chamanangwe kwa ajili ya kuanzisha Mradi wa ujenzi wa Ofisi za Maabara ya Wakala Pemba.
- Kamati inaishauri Wakala kutohilibika na baadhi ya wafanya biashara wasio waaminifu kwa kuhalalisha bidhaa ambazo hazina ubora na kupelekea kuharibu afya ya wananchi wanaotumia bidhaa hizo.
- Kamati inashauri Wizara kupitia Wakala wa Chakula, katika urasimishaji wa Bandari ya Shumba Mjini, Wizara kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi ihakikishe kuwa inaweka watendaji wa kutosha kufuatilia uingizaji wa dawa, chakula pamoja na vipodozi haramu vinavyoingizwa nchini kinyume na sheria.

**(F) ZIARA YA KAMATI HOSPITALI YA KIVUNGE**

Ni miongoni mwa Hospitali 10 za Wilaya zilizojenjwa chini ya Mradi wa Fedha za Ahuweni ya Uviko 19.

**CHANGAMOTO**

- Upungufu wa wafanyakazi pamoja na vifaa, kwa mfano: chumba cha wagonjwa mahututi (ICU), chumba cha upasuaji, chumba cha uchambuzi na maamuzi (triage), Wauguzi na Daktari wa mifupa.
- Ukosefu wa nyumba za wafanyakazi. Asilimia 80% ya wafanyakazi wanaishi mbali na hospitali katika makaazi yao. Makaazi ya wafanyakazi yaliyopo hospitalini hapo ni machakavu na ya zamani.

- Upungufu wa Huduma ya Damu. Kamati imebaini kuwa Hospitali ya Kivunge inauchangiaji mkubwa wa huduma ya damu kutoka kwa wananchi lakini imekua na upungufu kutokana na kuwa damu inayopatikana huwa haitoshelezi kwa kuwa inasambazwa katika vituo na hospitali nyengine zinazohitaji huduma hiyo.
- Kuwepo kwa muda mkubwa wa upatikanaji wa majibu ya vipimo.

**USHAURI/MAONI YA KAMATI**

- Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha inazifuatilia na kuzisimamia ipasavyo Kampuni Binafsi(outsource) zilizoingia makubaliano ya kushirikiana na Serikali kwa ajili ya kutoa baadhi ya huduma katika Hospitali za umma ili kuona huduma hizo zinatolewa kwa ubora na ufanisi.
- Kamati inaishauri Wizara kuharakisha kutoa majibu ya utoaji wa huduma wakati Kampuni za huduma za Outsouce wanapowasilisha mahitaji ya huduma zinazohitajika katika Hospitali na vituo vya afya zinazotoa huduma hizo.
- Kamati inashauri Wizara kuona umuhimu wa kutengeneza njia maalum itakayounganisha Jengo la huduma za mama na mtoto na Jengo jipya la Hospitali ya Kivunge.
- Kamati inashauri Wizara kuimarisha miundo mbinu mbali mbali ikiwemo uhaba wa mifereji na taa, katika jengo la huduma za mama na mtoto ili mama na Watoto waweze kupata huduma zinazostahili.
- Kamati inaishauri Wizara kurejesha upatikanaji wa huduma ya usafiri kwa wafanyakazi kwa kufanya malipo yanayodaiwa kutoka kwa kampuni ya Outsource ya SAIFEE ambayo ilisitisha kutoa huduma hiyo.

## 3. PROGRAMU KUU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA

Katika Programu hii, Kamati iliweza kufuatilia utekelezaji wa Mradi wa kuipandisha hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja kama ifuatavyo:

Hospitali ya Mnazi Mmoja inatekeleza MRADI WA ukarabati na utanuzi wa Hospitali hiyo KWA mashirikianon kati ya SMZ na Washirika wa Maendeleo. SMZ kupitia SerIkali ya SMT ilipata Mkopo wa jumla ya Dola za Kimarekani 42,800,000.00 ambapo Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Uchumi Barani Afrika (BADEA) inachangia kiasi cha $ 10,500,000.00, Mfuko wa kuweit wa maendeleo ya kiarabu (KFD) $ 13,600,000.00, Mfuko wa Saudia wa Maendeleo (SFD) $ 15,000,000.00 na Mfuko wa Serikali $ 3,700,000.00.

Shughuli zilizomo katika utekelezaji wa mradi huo ni pamoja na Uboreshaji wa majengo yaliyopo, ujenzi wa miundo mbinu mipya ya matibabu, ununuzi na ufungaji wa vifaa vya utibabu, samani za utibabu na zisizo za utibabu pamoja na mitambo ya kisasa ya hospitali. Kamati imeelezwa kuwa kupitia Mshauri Elekezi, kazi ya upembuzi yakinifu imeshafanyika, michoro na makadirio ya gharama za ukarabati wa majengo ya zamani na ujenzi wa majengo mapya pamoja na kukaa na wadau mbali mbali kwa mapendekezo ya mradi huo. Mradi umepangwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka minne 4 ,ambapo mwaka mmoja kwa shughuli za uendeshaji na miaka mitatu imeelekezwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi.

Lengo kuu la Mradi ni kupanua na kuimarisha huduma za afya kwa jamii ya wazanzibar kwa kuifanya Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja, Hospitali ya wazazi Mwembeladu na Hospitali ya wagonjwa wa akili Kidongochekundu.

**CHANGAMOTO**

- Ukosefu wa fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli za mradi
- Ufinyu wa eneo katika hospitali ya wazazi ya Mwembeladu unaoleta changamoto katika usanifu wa jengo jipya litakalokidhi mahitaji na utojai huduma nzuri za uzazi.
- Uwepo wa kanuni kali zilizowekwa na Mamlaka ya uhifadhi na Uendelezaji wa mji Mkongwe unazuia muundo wa kisasa wa majengo na ubomoaji wa majengo dhaifu ya kale ambayo yanaweza kuhatarisha

maisha ya watu hasa kwa watoa huduma na wagonjwa. Mfano jengo la viungo la ''PHYSIOTHERAPHY'' ambalo linapaswa kuvujnwa badala ya kukarabatiwa.

- Katika Hospitali ya MMH, huduma za maabara, changamoto kubwa in maji, Maji ambayo yanapatikana kwa sasa yana kiasi kikubwa cha chumvi kitu ambacho kinasababisha mashine hasa ya kemia kupata hitilafu mara kadhaa.
- Uhaba wa eneo la kuegesha magari (Parking), kwa hospitali ya MMH.

**USHAURI/MAONI YA KAMATI**

- Kamati inaungana na mapendekezo ya Wizara kwa Mamlaka ya Hifadhi na uendelezaji wa Mji Mkongwe ipunguze vikwazo kuhusu uhifadhi wa majengo ya kale ili kuruhusu uboreshaji wa miundo mbinu ya hospitali kabla ya majengo dhaifu kubomoka na kusababisha maafa kwa jamii.
- Kamati inaishauri serikali kulipia fidia kwa baadhi ya nyumba zilizo karibu na eneo la Hospitali ili kutoa nafasi ya ziada kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya kisasa ya Wazazi ya Mwembeladu.
- Katika utekelezaji wa Mradi wa Ukarabati wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa Utekelezaji wa Mradi huo unakuwa na ufanisi na unaanza kwa mujibu wa wakati uliopangwa. Kamati imebaini kuwa Serikali imekuwa na njema ya kutekeleza mradi huo lakini kumejitokeza baadhi ya vikwazo katika utekelezaji huo vikiwemo: kuchelewa kupatiwa fedha za Bajeti za uendeshaji katika kitengo cha usimamizi wa Mradi (PIU) jambo ambalo limesababisha deni kwa mujibu wa makubalinao ya utekelezaji wa mradi na taratibu za kisheria kuhusu matumizi mapya ya mji mkongwe zinazozuia kuvunja baadhi ya majengo ya zamani katika hospitali ya Mnazi mmoja kwa ajili ya matumizi ya Mradi.

- **ZIARA YA KAMATI KATIKA DIVISHENI YA AFYA YA AKILI HOSPITALI YA KIDONGO CHEKUNDU**

  Divisheni ya Huduma za Afya ya Akili Hospitali ya Kidongochekundu ni Hospitali Maalum inayotoa huduma kwa wananchi wa Zanzibar wanaosumbuliwa na matatizo ya Afya ya Akili. Huduma hii hutekelezwa chini ya Programu kuu ya kinga na elimu ya afya. Divisheni ya Huduma ya afya ya akili inatoa huduma ikiwemo:

1) Huduma za wagonjwa wa nje (OPD);
2) Huduma za wagonjwa maalum wanaotumia methadone (MAT clinic);
3) Huduma za kulaza:
   (a) Wagonjwa wa kawaida,
   (b) Watoto na vijana,
   (c) Wagonjwa waliopata uraibu (addiction).

**CHANGAMOTO -- DIVISHENI YA AFYA YA AKILI KATIKA HOSPITALI YA KIDONGO CHEKUNDU**

(a) Upungufu wa wafanyakazi wa TEHAMA na vifaa vyake ambao unasababisha huduma za HeMS kutofika maeneo yote ikiwemo ya wagonjwa wa ndani.

(b) Upungufu wa wafanyakazi katika divisheni kunadhorotesha upatikanaji upatikanaji wa huduma stahiki na kwa wakati. Hali inayopelekea wagonjwa kukaa mpaka mida ya baada ya kazi pamoja na wafanyakazi.

(c) Ufinyu wa bajeti ambao unapelekea kupunguza ufanisi wa wafanyakazi, ikiwemo bajeti ya vifaa muhimu vya kutolea huduma.

(d) Ufinyu wa jengo la huduma za nje (OPD), kusababisha kufanyia kliniki katika ofisi za uongozi wa divisheni.

(e) Uzio wa Hospital sio rafiki, hivyo kuruhusu mbwa kuingia eneo la hospital Pamoja na watu ambao wanaweza kusababisha wizi.

(f) Kushindwa kwa ufuatiliaji wa wagonjwa majumbani kwao ili kujua changamoyo zinazowakabili.

(g) Kutokuwepo kwa jengo la kulaza wagonjwa wanaokabiliwa na masuala ya kisheria (forensic psychiatry).

(h) Ukosekanaji wa sare (uniform) pamoja na uhaba wa magodoro ya kulalia kwa wagonjwa.

(i) Kukosekana kwa maabara katika na vitendea kazi vyake katika hospitali na kupelekea kuchelewa kupata majibu ya vipimo kutoka Hospitali ya Mnazi Mmoja.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

**a.** Kamati inapendekeza kwa Serikali pamoja na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuitengea fungu maalum la fedha za uendeshaji wa Divisheni ya Afya ya Akili Hospitali ya Kidongo Chekundu na sio vyema kutegemea fedha kwa asilimia kubwa kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa ajili ya uendeshaji wa hospitali hiyo bila ya kutenga fedha yoyote kutoka katika bajeti yetu ya Serikali.

**b.** Kamati inaishauri Serikali kukaa na Wizara ya Afya kuliangalia kwa kina suala la ukosefu wa watendaji wa kudumu wa Serikali katika Divisheni ya Afya ya Akili Hospitali ya Kidongo Chekundu ambao wanatoa huduma za matibabu kwa wagonjwa wanaofika hapo kwani Kamati imeshangazwa kuona watendaji waliopo asilimia kubwa wameajiriwa kwa mkataba.

**c.** Kamati pia inaishauri Serikali kupitia Tume ya Utumishi Serikalini kulitafutia ufumbuzi wa haraka suala la kuwaondolea watendaji wa afya posho la mazingira hatarishi (risk allowance) kwa watendaji wa divisheni pamoja na hospitali nyengine.

**d.** Vile vile, Kamati inashauri Serikali kuweka utaratibu wa kuwaendeleza wafanyakazi kwa kuwapatia nafasi za mafunzo kazini ya muda mfupi na muda mrefu ili kuzalisha wataalamu bingwa wa kada tofauti za afya ikiwemo Afya ya Akili.

**e.** Kamati inaishauri Wizara kuangalia namna itakayoweza kuifanya Hospitali ya wagonjwa wa akili kuweza kujitegemea au kuwa na kasma ya Fungu maaulum la matumizi. Kamati imebaini kuwa kuna urasimu mkubwa unaopelekea watendaji katika hospitali hiyo kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi kutokana na kuchelewa kupata mahitaji ya huduma muhimu za hospitali ambazo huduma hizo mpaka zitolowe kupitia Hospitali ya Mnazimoja.

**f.** Kamati inashauri Wizara kuwatafutia Uniform(sare) wagonjwa walipo kituoni hapo ili iwe rahisi kwao kutambulika na jamii pindi wakitoroka katika uzio huo.

**g.** Kamati inaitaka Wizara ya Afya wawatafutiye magodoro yaliyo madhubuti ambayo sio rahisi kuharibiwa na wagonjwa kwa ajili ya kuweka wodini kwa ajili ya matumizi ya kulalia kwani kamati imebaini kuwa wagonjwa wanalala chini kutokana na baadhi yao kuyaharibu kwa kuyachana kutokana na kua magodoro hayo siyo imara.

**h.** Kamati imebaini kuwa licha ya kuwepo Maabara kwa ajili ya vipimo katika hospital ya wagonjwa wa akili lakini Maabara hiyo haifanyi kazi na kupelekea huduma hizo kufikishwa katika hospitali ya mnazimoja kwa uchunguzi. Hivyo Kamati inashauri Wizara kuhakikisha inaimarisha huduma za maabara katika Hospitali hiyo ili kupunguza usumbufu kwa wagonjwa kufuata huduma hizo nje.

**i.** Kamati inashauri Wizara kuhakikisha kuwa inakuweka Databezi ya wagonjwa wa akili inayoeleweka ili tawimu za wagonjwa hao kuweza kufahamika.

**j.** Kamati imebaini kuwa wafanyakazi wengi wanaotoa huduma katika Hospitali ya Wagonjwa wa akili ya Kidongo Chekundu ni wanawake, hali ambayo inaweza kuleta athari kwa wafanayakazi hao katika kuwahudumia wagonjwa wa aina hiyo. Hivyo Kamati inashauri kurejeshwa utaratibu wa zamani kuwekwa walinzi maalum wa kiume

watakaoweza kusaidia kuwadhibiti wagonjwa hao inapotokezea haja ya kufanya hivyo.

**k.** Kamati inaishauri Wizara kuuboresha uzio wa hospitali hiyo ili kuhakikisha kuwa wanazuia uharibifu wa vijana wanaodaiwa kutumia madawa ya kulevya ambao wamekuwa wakikaa nje ya geti la Hospitali pamoja na wanyama wakali wanaingia kutokana na ubovu wa uzio huo

## 4. PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI WA URATIBU WA WIZARA

Programu hii inahusika na usimamizi wa rasilimali watu, rasilimali fedha, manunuzi, sheria na shughuli nyengine za uendeshaji wa Wizara. Aidha, ina jukumu la kuandaa na kusimamia Sera, Miongozo, Mipango pamoja na Kuratibu taarifa za Afya

Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2023, Idara ya Uendeshaji na Utawala ilikadiriwa kuingiziwa jumla ya shillingi 5,439,051,730/= Kati ya fedha hizo shilling 2,152,039,054/= zilingizwa kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 79.9 na shilling 2,500,718,856.00/= kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji sawa na asilimia 91.1.

## CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WIZARA YA AFYA KWA UJUMLA

i. Uingiaji usioridhisha wa fedha za kuendesha hospitali na kupelekea huduma nyingi za hospitali kuzorota.
ii. Upungufu wa rasilimali watu katika kada mbali mbali za afya wakiwemo madaktari, wataalamu wa ganzi na usingizi, wauguzi n.k pamoja na watendaji wengi wa hospitali kutokuwa na ujuzi wa kutosha kwenye taaluma zao.
iii. Kurejea na kuenea kwa kasi homa ya Malaria.
iv. Kuwepo kwa vyanzo vichache vya mapato katika sekta ya afya ambavyo hutoa mchango mdogo katika utoaji wa huduma za afya nchini.

v. Uchakavu wa baadhi ya vituo vya Afya vya Daraja la Kwanza ambapo kunapelekea baadhi ya huduma kutotolewa ipasavyo.
vi. Ukosefu wa miundombinu ya TEHAMA hasa kwenye vituo vya afya.
vii. Kuwepo kwa ongezeko kubwa la fedha za ziada (variations) katika miradi mingi inayotekelezwa kupitia fedha za UVIKO - 19 hali iliyopelekea Wizara kuwa na ongezeko kubwa la fedha katika miradi hiyo kinyume na Bajeti ya fedha za awali zilizopangwa.
viii. Kuwepo kwa uwezo mdogo wa baadhi ya watendaji katika kuibua na kusimamia miradi kutokana na kutokuwa na kitengo maalum cha wizara kinachosimamia utekelezaji wa miradi.
ix. Kuchelewa kwa malipo ya wakandasari kutoka Wizara ya Fedha na Mipango
x. Wizara Kupangiwa kiwango kikubwa cha makusanyo yatokanayo na vyanzo vya mapato ya ndani kinyume na hali halisi ya vyanzo vya mapato vilivyopo, hali inayopelekea kutokuwepo kwa ufanisi katika makusanyo wakati wa utekelezaji wa bajeti husika.
xi. Kuchelewa kukamilika kwa Mradi wa Ujenzi wa Nyumba wa watumishi katika Hospitali ya Abdalla Mzee na Micheweni kwa Pemba na Hospitali ya Kivunge kwa Unguja.
xii. Kuchelewa kumalizika kwa baadhi ya Miradi ya Hospital za Wilaya ndani ya Wakati uliopangwa.
xiii. Kuchelewa kuanza kwa ujenzi wa Hospital ya Wete.
xiv. Kuharibika mara kwa mara mashine na vifaa tiba kama vile mtambo wa kuzalisha gesi ya oxygeni na mtambo wa kuchomea taka
xv. Uuzwaji holela wa dawa za asili katika maeneo ya misikiti, masoko na sehemu za wazi jambo ambalo ni kinyume na utaratibu.
xvi. Kutokamilika kwa mfumo wa uwekaji takwimu za Uviko 19 (Chanjo Covid system).

xvii. Ukosefu vifaa vya kutendea kazi kama vile mashine ya dialysis ndani ya ICU, PET scan, mashine ya kukaushia nguo mashine za kupikia vifaa (autoclove),

xviii. Kukosekana baadhi ya Huduma na utaalamu katika Hospital ya Mnazi Mmoja kama Bone marrow biopsy.

xix. Kukosekana kwa tanuri la kuchomea taka kwa hospital ya MMH ambapo taka hatarishi zinaendelea kutupwa katika jaa kuu la Kibele.

xx. Uchache wa vitendea kazi na kuharibika mara kwa mara kwa computer za Bohari Kuu ya Dawa Unguja na Pemba jambo ambalo limepelekea kushindwa kukamilisha kazi kwa wak

xxi. Wadau wengi wa tiba asili hawana taaluma ya kutosha hivyo hupelekea ukiukwaji mkubwa wa maadili na miiko ya Tiba asili.

xxii. Ukosefu wa Internet katika vituo vya afya hivyo kusababisha utumiaji wa mfumo na kukosa taarifa sahihi (data qua

xxiii. Kukosekana kwa baadhi ya taarifa za afya ya jamii kwa baadhi ya manispaa.

xxiv. Kucheleweshewa utaratibu wa manunuzi kwenye mambo ya uendeshaji kwa Bohari mfano ununuzi wa mafuta, vifaa vya magari pamoja na Forkolift.

xxv. Ripoti na maombi ya dawa kutoka vituoni zinakuwa na makosa mengi na kusababisha kurudishwa kwa wahusika ili kurekebishwa jambo linalozorotesha shughuli za usambaza

xxvi. Uchache wa wafanya kazi wa kada mbalimbali katika Bohari kuu ya Dawa Vitongoji Pemba kama vile;(Wafamasia, Fundisanifu Madawa, na Afisa Tehama).

xxvii. Uchache wa wasaidizi wa ndani ya ghala la madawa(Store Attendants) na wakati mwingine kutumika kwa wasaidizi hao kutekeleza kazi nyengine za nje ya Bohari .

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

i. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuwaingizia fedha kwa wakati Wizara ya Afya kwa ajili ya kuweza kutekeleza majukumu yao kama walivyojipangia kwenye bajeti, kwani kuchelewa kupatikana kwa fedha hizo kunasababisha kuzorota kwa shughuli nyingi za uendeshaji wa hospitali pamoja na vituo vya afya.

ii. Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha inazifuatilia na kuzisimamia ipasavyo Kampuni Binafsi(outsource) zilizoingia makubaliano ya kushirikiana na Serikali kwa ajili ya kutoa baadhi ya huduma katika Hospitali za umma ili kuona huduma hizo zinatolewa kwa ubora na ufanisi.

iii. Kamati inaishauri Wizara kuharakisha kutoa majibu ya utoaji wa huduma wakati Kampuni za huduma za outsouce wanapowasilisha mahitaji ya huduma zinazohitajika katika Hospitali na vituo vya afya zinazotoa huduma hizo.

iv. Kamati inaipongeza serikali kwa kuanzisha mfuko wa bima ya afya ambapo kamati inaisisitiza Wizara kusimamia vyema upatikanaji wa huduma hii muhimu ya afya ikiwemo upatokanaji wa dawa ipasanyo ili kuona malengo ya Serikali kwa wananchi wake juu ya mfuko huo yanafikiwa kwa ufanisi na wananchi wanafaidika nao.

v. Kamati inaipongeza Wizara ya Afya kwa kufanya ukarabati wa Vituo vya Afya 11 vya Daraja la Kwanza na kukamilisha Ujenzi ya wa baadhi Hospitali 10 za Wilaya na 1 ya Mkoa nayo kuendelea na ujenzi kwa lengo la kutoa huduma bora na za kisasa.

vi. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuwashirikisha kikamilifu watendaji wa Wizara husika wakati wa kupanga mafungu ya Mapato ya Wizara pamoja na Taasisi zake zote

zinazokusanya kupitia vyanzo vyake vya ndani ili kukadiria bajeti yenye uhalisia kwa mwaka husika na sio bajeti ya kufikirika.

vii. Kamati inaishauri Serikali inapotekeleza Miradi mikubwa ya Maendeleo kuwashirikisha kikamilifu wataalamu wa Wizara husika ili kuepusha changamoto ya matumizi ya ziada ya fedha za Serikali kwa kuwepo ongezeko la kazi za ziada nje ya mikataba ya awali na Wakandarasi.

viii. Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kuweka miundombinu ya TEHAMA kwenye Vituo vyote vya Afya kwa Unguja na Pemba ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa sahihi za huduma za afya katika vituo hivyo.

ix. Kamati inaishauri Wizara kufuatilia kibali kupitia Tume ya Utumishi Serikalini cha uajiri wa wafanyakazi wapya wa kada mbali mbali za afya kila inapohitajika ili kupunguza changamoto ya ukosefu wa wataalamu na madaktari katika hospitali zetu.

x. Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kuwa na mpango madhubuti wa muda mfupi na muda mrefu wa kuwasomesha na kuwaendeleza madaktari, wauguzi na wafanyakazi wengine waliopo katika hospitali zetu ili kuwaongezea ujuzi katika kazi zao na kuwa na wataalamu wa kutosha wanaokwenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknologia katika sekta ya afya.

xi. Kamati inaishauri Wizara kufuatilia ipasavyo ukamilikaji wa Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za watumishi katika Hospitali ya Abdalla Mzee na Micheweni kwa Pemba na Hospitali ya Kivunge kwa Unguja ili kuwaondoshea usumbufu watumishi wanaofanya kazi kwenye hospitali hizo ambao wanaishi mbali na vituo vyao vya kazi.

xii. Kamati inaishauri Serikali kuwasiliana na Wafadhili wa ujenzi wa Hospitali ya Wete ili Hospitali hiyo ijengwe kwa mujibu wa Makubaliano.

xiii. Kamati inaipongeza Wizara kuona umuhimu wa kuanzishwa chuo cha afya Pemba. Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na wadau wa

maendeleo kufuatilia changamoto inazozikabili chuo hicho ili kiweze kutoa huduma kwa ufanisi.

xiv. Kamati inaishauri Wizara kuzingatia ufanyaji wa mitihani ya Uuguzi kwa upande wa Pemba kufanyika Pemba badala ya watihaniwa kufuata ufanyaji wa mitihani hiyo Unguja hali ambayo imeelezwa kuwa ni usumbufu.

xv. Kamati inaishauri Wizara kuwa na mpango maalum wa kudhibiti Uuzwaji holela wa dawa za asili katika maeneo ya misikiti, masoko na sehemu za wazi jambo ambalo ni kinyume na utaratibu.

xvi. Kamati inaipongeza Wizara kuwa Mpango wa kujenga kituo rasmi cha kuangamiza dawa zilizopitwa na wakati.

xvii. Kamati inaishauri wizara kusaidia katika uendeshaji wa maabara ya jamii(PHL-Ide) Pemba, badala ya kuwaachia wahisani pekee sambamba na kuzisimamia Maabara hizo katika kufanya tafiti za maradhi ya miripuko ambayo yameonekana kuibuka mara kwa mara katika jamii . Kamati imebaini kuwa maabara hizo zinauwezo mkubwa lakini tafiti zinazofanywa hazilingani na uwezo wa maabara hizo.

**xviii.** Kamati inaishauri wizara kuchukua juhudi zaidi katika utoaji wa Huduma za Kumaliza Malaria Zanzibar ambayo imeonekana kurejea kwa kasi.

**HALI YA KIFEDHA KWA UJUMLA.**

Wizara ya Afya katika mwaka wa fedha 2023/2024 inakadiriwa kutumia kiasi cha shilingi 189,379,436,000/= (Fungu HO1) na Shilingi 49,772,000,000/= kwa matumizi ya Hospitali ya Mnazi Mmoja (Fungu HO2).

Aidha, Wizara inakadiriwa kukusanya shilingi 5,751,881,000/= na shilingi 1,348,585,000/= kwa Hosptali ya Mnazi Mmoja.

**UTEKELEZAJI**

Kwa upande utekelezaji wa kifedha kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2023, Wizara ya Afya (Fungu H01) ilikadiriwa kutumia

shilingi 95,189,718,000/= ikijumuisha shilingi 27,874,604,078/= kwa ajili ya mishahara; shillingi 31,515,893,190/= kwa kazi za kawaida (OC); shillingi 2,961,244,962/= kwa Ruzuku na shilling 32,837,975,770/= kwa kazi za Maendeleo.

**Matumizi**

Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2023, Wizara ya Afya (H01) iliingiziwa na kutumia jumla ya shillingi 71,190,091,122/= sawa na asilimia 74.8 ya matumizi ya fedha zilizoingizwa na kutumia. Kati ya fedha hizo shillingi 33,823,820,459/= kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 121.34. Shillingi 19,716,133,363= kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji sawa na asilimia 62.6 na shillingi 2,546,474,599/= kwa ajili ya ruzuku sawa na asilimia 86. Aidha, shillingi 15,103,662,700/= sawa na asilimia 46 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za maendeleo, kati ya fedha hizo shillingi 12,091,626,708= ziliingizwa sawa na asilimia 45.6 kutoka Serikalini, na shillingi 1,454,699,600/= sawa na asilimia 26.9, kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na mkopo 1,557,336,392.87 zilingizwa sawa na asilimia 174.04.

Hali ya Kifedha kwa upande wa Hospitali ya Mnazi Mmoja(H02),

Fedha za matumizi zilizopatikana kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2023/2024, ni jumla ya shilingi 17,001,527,212/= ambapo shilingi 11,061,527,212,/= kwa mishahara ya wafanyakazi, shilingi 610,000,000/= kwa uendeshaji wa Hospitali na jumla ya shilingi 5,330,000,000/= ni kwa malipo ya kampuni ya utowaji wa huduma za dawa (BARIKI) na huduma za uchunguzi (NSK). Aidha, matumizi ya mradi wa kupandisha Hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja ni jumla ya shilingi 1,045,951,391/= kwa malipo ya ununuzi wa vifaa tiba na mashine za hospitali pamoja na ununuzi wa computer kwa uendelezaji wa mfumo wa kielektroniki hadi wodini. Pia matumizi ya mradi wa Ukabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja (BADEA, SFD pamoja na KFD), umepokea jumla ya shilingi 846,592,500/= kutoka kwa washirika wa Maendeleo ambapo jumla ya shilingi

573,592,500/= ni kwa malipo ya mshauri elekezi na shilingi 273,000,000/= ni kwa mishahara ya wafanyakazi wa mradi (PIU).

**Mapato**

Wizara ya ilikadiriwa kukusanya jumla ya Shillingi 2,839,242,168/= kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2023, Wizara ilifanikiwa kukusanya mapato kutoka vyanzo mbali mbali vya Wizara (H01), Hadi kufikia Disemba 2023, jumla ya shilling 1,473,019, 325/= zimekusanywa sawa na asilimia 52.

Hospitali ya Mnazi Mmoja (H02), ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 676,688,369/= Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2023 kupitia vyanzo vya malipo ya Huduma za Afya, Huduma za Haraka (Fast Track), huduma za Bima na malipo ya wanafunzi wa kigeni. Hadi kufikia Disemba, 2023 jumla ya shilingi 357,166,867.85/= zimekusanywa sawa na asilimia 53.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ni sekta ambayo inahusika na Maendeleo ya Jamii ambayo yanazingatia Usawa wa Kijinsia wa wananchi. Wizara ina dhamana ya kuhakikisha inainua hali za kijamii na kiuchumi kwa wanawake, sambamba na kulinda haki za wazee, watoto, na jamii kwa ujumla kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo kutoka jumuiya za kitaifa, kikanda na kimataifa, sekta binafsi na asasi za kiraia.

Utekelezaji wa shughuli za Wizara unazingatia mpangilio wa Programu Kuu tatu na Programu ndogo tatu kama ifuatavyo:-

i. Programu Kuu ya Hifadhi ya Jamii - PH0401
ii. Programu kuu ya Uratibu na Utawala - PH0402
    a. Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji,
    b. Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti
    c. Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji ofisi Kuu Pemba
iii. Programu kuu ya Maendeleo Jamii, Jinsia na Watoto - PH0403

Shughuli za programu hizo hutekelezwa kupitia Idara zifuatavyo:-

1. Idara ya Ustawi wa Jamii na Wazee.

2. Idara ya Uendeshaji na Utumishi.

3. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

4. Idara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

5. Ofisi Kuu Pemba.

Wizara inaendelea kusimamia na kutekeleza malengo ya Dira ya 2050 ya Zanzibar, Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020 – 2025, Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar 2021-2026, Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs 2030), Agenda ya Afrika (2063) na kusimamia Sera ya Jinsia ya Zanzibar 2016, Sera ya Hifadhi ya Jamii 2014, Sera ya Maendeleo ya Mtoto 2002, Sheria ya Mtoto Nambari 6 (2011) na Sheria ya Wazee Nambari 2 (2020).

**UPATIKANAJI WA FEDHA**

Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Mendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imekadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 20,000,000 kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali . Aidha Wizara imekadiriwa kutumia jumla ya shilingi 9,887,311,000 kati ya fedha hizo shilingi 7,170,000,000 sawa na asilimia 72.52 mchango wa serikali na shilingi 580,990,000/= sawa ana asilimia 5.87 ruzuku kutoka kwa washirika wa maendeleo. Fedha za miradi ni shilingi 2,136,321,000/= saw ana asilimia 21.61

Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2023, Wizara ilipanga kupatiwa shilingi 5,647,261,967.81 (Unguja shilingi 5,169,030,837.81 na Pemba shilingi 478,231,130). Hadi kufikia mwezi wa Disemba 2023, Jumla ya shilingi 2,899,174,071 (Unguja shilingi 2,480,017,655 na Pemba shilingi 419,156,416) zimepatikana, sawa na asilimia 40.64, kati ya fedha hizo shilingi 530,048,791 (Unguja shilingi 409,048,791 na Pemba shilingi 121,000,000) zimetumika kwa matumizi ya kawaida ya ofisi, shilingi 1,833,031,752 (Unguja shilingi 1,570,875,336 na Pemba shilingi 262,156,416) kwa malipo ya mishahara, shilingi 226,500,000 (Unguja shilingi 190,500,000 na Pemba shilingi 36,000,000) msaada ulipokewa kutoka wahisani kwa wazee na shilingi 309,593,528 ruzuku kutoka kwa washirika wa maendeleo.

## UTEKELEZAJI WA PROGRAMU

## 1. PROGRAMU YA HIFADHI YA JAMII (PH0401)

Programu hii ina jukumu la kuratibu na kusimamia upatikanaji wa haki kwa makundi yenye mazingira magumu zaidi kwa kuimarisha mifumo ya Hifadhi ya Jamii ili kupunguza kiwango cha umasikini hapa Zanzibar.

Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara imetenga shilingi 2,596,974,000 sawa na asimia 26.27 ya bajeti ya wizara kwa ajili ya utekelezaji Programuu hii. Shilingi 1,500,000,000 kwa ajili ya mradi wa maendeleo na shilingi 1,096,974,000/= kwa ajili ya shughuli zilizotengwa na program hii.

## CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU

- Kuwepo kwa uchakavu wa majengo ya muda mrefu ya hifadhi ya wazee
- Kuwepo kwa utaratibu usioridhisha wa upatikanaji wa Pencheni jamii kwa wazee
- Kuendelea kuibuka kwa kesi mbali mbali za udhalilishaji wa Watoto
- Kuwepo kwa utitiri wa nyumba zisizorasmi za kulelea Watoto.
- Kutokuwepo kwa uzio katika nyumba za wazee Welezo na Limbani.

## MAONI /USHAURI WA KAMATI.

- Kamati inaishauri Wizara kukamilisha mpango wa ukarabati wa majengo hayo ya makaazi ili wazee hao waweze kuwa na makaazi bora zaidi.
- Kamati inaishauri Wizara kuimarisha huduma katika kuwasaidia watu wenye mazingira magumu Zaidi ambao wapo mitaani hawatambuliki na wanahitaka uhitaji Zaidi.
- Kamati inapongeza Wizara kwa kuendelea kuwapatia wazee huduma za kiustawi ikiwa ni chakula, mavazi, malazi, matibabu na fedha za kujikimu ambapo jumla ya Wazee 65 waliopo katika makaazi ya wazee [Welezo 34 (wanawake 11 na wanaume 23), Sebleni 21 (wanawake 13

wanaume 8) na Limbani 10 (wanawake 3 na wanaume 7)] wamepatiwa huduma hizo.

- Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kusambaza vitambulisho 19,715 kwa wazee kupitia Ofisi za Wakuu wa Wilaya zote za Unguja na Pemba. Vitambulisho vyengine vinaendelea kwenye hatua ya kuchapishwa baada ya taarifa za wazee husika kuingizwa katika mfumo wa Wakala wa Matukio ya Kijamii.
- Kamati inapongeza Wizara kwa kushirikiana na wadau mbali mbali imeadhimisha Siku ya Wazee Duniani ambayo hufanyika tarehe 1 Oktoba ya kila mwaka. Kauli mbiu ya mwaka huu ni "Uthabiti wa Wazee kwenye dunia yenye Mabadiliko".
- Kamati inaishauri Wizara kuendelea kufanya uhakiki wa wazee wapya na kusajiliwa katika Mpango wa Pensheni Jamii.
- Kamati inaishauri Wizara kueendelea kuwatunza na kuwahudumia watoto katika nyumba ya kulelea watoto Mazizini. Sambamba na kuhifadhi misaada mbali mbali ya vifaa na fedha kutoka kwa watu binafsi, taasisi za jamii, na taasisi za Serikali kwa ajili ya kusaidia huduma za kituo hicho.

## 2. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA (PH0402)

Programu hii ina jumla ya programu ndogo tatu, ambazo ni Utawala na Uendeshaji, Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti na Uratibu wa Wizara Pemba.

Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2023 ilipanga kutekeleza shughuli zifuatazo: - Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara; ii. Kununua nyenzo pamoja na vifaa vya Wizara; iii. Kuendelea kuweka mazingira mazuri kwa watumishi pamoja na kuwapatia maslahi yao.

Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara imetenga shilingi 5,648,868,500 sawa na asimia 57 ya bajeti ya wizara kwa ajili ya utekelezaji Programuu hii. Shilingi 3,170,000,000 kwa ajili ya mishahara, shilingi 1,728,868,500 kwa ajili ya matumizi ya ofisi unguja na shilingi 750,000,000 kwa uratibu na uendeshaji shughuli Pemba.

**CHANGAMOTO**

Kamati katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa Programu hii imebaini changamoto zifuatazo:

- Wizara kuendelea kukodi jengo la ofisi kwa gharama kubwa ambapo kwa muda wa miezi sita imefanya malipo ya jumla shilingi 35,962,917 ya kodi ya jengo na shilingi 22,914,072 zilitumika kwa ajili ya huduma za mtandao (internet) katika jengo hilo.
- Ongezeko la malalamiko ya wazee wanaonufaika na Mpango wa Pencheni Jamii.
- Upatikanaji mdogo wa fedha za matumizi ya kawaida.
- Kukosekana kutambuliwa wazee wa mitaani na mashamba jambo ambalo linawakosesha wazee hao kupata haki yao hiyo.

**MAONI/USHAURI WA KAMATI**

i. Kufuataia kuwepo kwa Ongezeko la malalamiko yanayowasilishwa na wazee wanaonufaika na Mpango wa Pencheni Jamii, Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na Wadau wake kubuni mbinu muafaka zitakazoweka uratibu bora zaidi utakaohakikisha kuwa taarifa za wazee watarajiwa zinapatikana na kuingizwa katika mfumo endelevu wa kielektronik, sambamba na kurejeshwa kwa utaratibu wa malipo ya Pencheni kwa wizara husika. Hatua hiyo itasadia kuondoa malalamiko mengi kutoka kwa wazee wastaafu ya kuwepo kwa usumbufu mkubwa wa utaratibu wa kupata malipo ya pencheni zao.

ii. Kamati inaishauri serikali kupitia Wizara ya fedha na mipango kuzingatia kuipatia ipasavyo Wizara ya maendeleo ya ustawi wa jamii mgao wa fedha za matumizi ya kawaida ili wizara iweze kuendesha shughuli zake kwa ufanisi.

iii. Kamati inaipongeza wizara kwa kuendeleza mashirikiano na uongozi wa Kijiji cha SOS. Taasisi hiyo imekuwa na mchango mkubwa kwa wizara katika kuhakikisha kuwa malengo ya wizara na ya Kijiji cha SOS yanafikiwa ipasavyo.

iv. Kamati inaishauri Wizara kukamilisha Mpango wake wa kuwa na jengo la kudumu kwa ajili ya ofisi ya Wizara, kuendelea kukodi kwa ajili ya kuendesha shughuli za ofisi kunapelekea kuwa gharama na matumizi makubwa ya fedha.

## 3. PROGRAMU YA MAENDELEO YA JAMII NA JINSIA (PH0403)

Programu hii ina programu ndogo moja ambayo ni Uratibu Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto inatekeleza shughuli zake kwa kufuata sheria, kanuni na miongozo inayo lenga jinsia, watoto na kuwawezesha wanawake wajasiriamali, kupinga Ukatili na Udhalilishaji pamoja kuwajengea uwezo Wanawake kuingia kwenye nafasi za Uongozi.

Katika kipindi cha Julai-Disemba 2023, Programu hii ilipanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuandaa mpango kazi mpya wa kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto (NPA-VAWC 2023-2028);

ii. Kuhamasisha na kuelimisha jamii juu ya kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto katika ngazi zote;

iii. Kuratibu na kuhamasisha utekelezaji wa Ahadi za Nchi juu ya Kizazi Chenye Usawa;

iv. Kuratibu, kuwawezesha na kuwaunganisha wanawake na fursa mbalimbali;

v. Kuratibu, kuwezesha na kuimarisha mabaraza ya watoto katika ngazi zote;

vi. Kuhamasisha na kuimarisha malezi ya pamoja; na vii. Kutekeleza shughuli za kubadili wanawake kuingia kwenye nafasi za uongozi.

Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara imetenga shilingi 1,641,468,500 sawa na asimia 17 ya bajeti ya wizara kwa ajili ya utekelezaji Programuu hii. Shilingi 564,157,500/= mchango wa serikali ,shilingi 1,077,311,000/= ruzuku za washirika wa maendeleo kwa ajili yha uendeshaji na mradi wa kupinga ukatili na udhalilishaji na kubadilisha wanawake kuingia katika nafasi za uongozi.

**CHANGAMOTO**

Kamati katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa Programu hii imebaini changamoto zifuatazo:

- Kutokamilika kwa mpango kazi mpya wa kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto (NPA-VAWC 2023-2028)
- Uwezo mdogo wa vikundi vingi vya wajasiri amali wanawake katika kujiendeleza kiuchumi
- Kuhitajika kwa elimu zaidi ya kuhamasisha Jamii kuhusu mapambano dhidi ya udhalilishaji
- Wizara kukosa Bajeti maaalum ya kuendesha mabaraza ya watoto
- Kutokamilika kwa Muongozo Mpya wa Mabaraza na klabu za watoto
- Utaratibu mzima usioridhisha wa malipo ya pencheni jamii kwa wazee
- Uchache wa wanachama katika Mabaraza ya watoto.
- Kutokamilika kwa uandaaji wa Sera ya Mtoto, Kanuni na Muongozo wa Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi.

- Baadhi ya jamii kutokuwa tayari kuwashirika ipasavyo Watoto katika Mabaraza ya Watoto.
- Kuosekana kwa kanuni katika Sheria ya Wazee.
- Kukosekana kwa bajeti katika utekelezaji wa Mpango wa Pencheni Jamii sambamba na muongozo wake.
- Kukosekana kwa mafunzo ya kujengewa uwezo kwa maafisa wanaohudumu katika Mpango wa Pencheni jamii.

**MAONI /USHAURI /MAPENDEKEZO YA KAMATI**

- Kamati inaishauri Wizara kukamilisha kwa wakati uandaaji wa Mpango kazi mpya wa kitaifa wa kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto katika kuanzisha juhudi mpya za mapambano dhidi ya udhalilishaji.
- Kamati inaipongeza Wizara kwa juhudi zake za kuendelea kuelimisha na kuhamasisha Jamii katika maeneo tofauti ya Unguja na Pemba kuhusu mapambano dhidi ya udhalilishaji. Uelimishaji huo ulijumuisha Shehia, Madrasa, Skuli, nyumba za ibada, Timu za wanaume wa mabadiliko, vikundi vya mazoezi, vyombo vya habari pamoja na makundi mbalimbali ya wanajamii juu ya kujikinga na kupambana dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.
- Kamati inaipongeza Wizara kwa kufanya utafiti wa tathmini ya jinsia na UKIMWI kwa kufanya mikutano na wadau kutoka Taasisi za Serikali na Asasi za kiraia (NGOs) kwa Unguja na Pemba, Tathmini ambayo ilibaini kuwepo na changamoto mbali mbali ikiwemo za kisheria katika masuala ya jinsia, kisera na upatikanaji wa huduma za ushauri nasaha kwa wahanga wa matukio ya udhalilishaji na UKIMWI.
- Kamati inaishauri Wizara kuendelea kuwakutanisha Wajasiriamali Wanawake ili waweze kuwa na sauti ya pamoja na kuibua changamoto zao

na kuziripoti katika ngazi mbali mbali ili kupatiwa ufumbuzi, ikiwemo kuwatafutia masoko, mitaji na fursa za elimu ya ujasiriamali.

- Kamati inaishauri Wizara kukamilisha maboresho ya maeneo yenye changamoto katika utekelezaji wa Sheria ya Mtoto pamoja na kuandika rasimu ya sheria hiyo ili kuweza kuwa na rasmi ya mtoto.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO.

Wizara hii ni miongoni mwa wizara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Uongozi wa Awamu ya Nane hivyo wizara hii imeundwa na sekta huu nne ambazo ndizo zinazo unda wizara ya habari vijana utamaduni na michezo na sekta yenyewe ni kama hizi zifuatazo:-

*(i)* Sekta ya Habari;
*(ii)* Sekta ya Vijana;
*(iii)* Sekta ya Utamaduni; na
*(iv)* Sekta ya Michezo.

**SEKTA YA HABARI**

*(a)* Idara ya Habari na Maelezo;
*(b)* Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC);
*(c)* Tume ya Utangazaji Zanzibar;
*(d)* Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar (ZGPA);
*(e)* Kampuni ya Kuunganisha na Usambazaji wa Maudhui Zanzibar (ZMUX);
*(f)* Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar.

**SEKTA YA VIJANA**

*(i)* Idara ya Maendeleo ya Vijana;
*(ii)* Baraza la Vijana Zanzibar.

**SEKTA YA UTAMADUNI**

*(i)* Idara ya Utamaduni;
*(ii)* Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni;
*(iii)* Baraza la Kiswahili (BAKIZA).

**SEKTA YA MICHEZO**

*(i)* Idara ya Michezo;

*(ii)* Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar (BTMZ);

*(iii)*Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;

*(iv)* Idara ya Utumishi na Uendeshaji

Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara imepanga kutekeleza Program Kuu (4) zifuatazo:

i. Programu kuu ya maendeleo ya habari, utangazaji na uchapaji- **PJ0301**
ii. Programu ya maendeleo ya vijana-**PJ0302**
iii. Programu ya maendeleo ya utamaduni, sanaa na michezo - **PJ0304**
iv. Programu ya uendeshaji na mipango katika sekta ya habari, vijana, utamaduni na michezo - **PJ0304**

## 1. PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA HABARI, UTANGAZAJI NA UCHAPAJI

Programu hii inaundwa na Programu Ndogo mbili ambazo ni Upatikanaji na Usambazaji wa Habari na Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji.

Shughuli kuu zinazotolewa ni Urushaji wa Vipindi na Matangazo, kupitia TV na Redio, Utoaji wa Taarifa, Picha, Makala, Filamu na Sinema, Utoaji wa Magazeti, Usambazaji wa Maudhui, Kudhibiti na Kusimamia Shughuli za Utangazaji kupitia Sera na Sheria za Habari na Utangazaji, Kusimamia Shughuli za Uchapaji pamoja na kudhibiti na kusimamia shughuli za Vituo vya Utangazaji kupitia Sera na Sheria za Utangazaji.

Katika mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya Tanzania Shilingi 9,612,311,000/= zimepangwa kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

Kamati katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa Progaramu hii, Kamati imeweza kutemblea taasisi mbali mbali ili kufahamu mafanikio na changamoto na kuweza kuishauri Serikali kama ifuatavyo:

## A. SHIRIKA LA MAGAZETI ZANZIBAR (SMS)

Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar limeanzishwa chini ya Sheria Nambari 11 ya mwaka 2008. Shirika la Magazeti ya Serikali (SMS) linachapisha magazeti manne (4) ambayo ni gazeti la siku (Zanzibar Leo, Magazeti ya kila wiki (Zanzibar Mail na Zanspoti) na gazeti la Zanzibar Leo Jumapili ambalo hutolewa kila siku Jumapili. Magazeti haya husambazwa Zanzibar nzima na Mikoa 22 ya Tanzania Bara kwa lengo la kusambaza taarifa zenye kuelimisha kuhusu mambo mbali mbali ya nchi, burudani na michezo.

**KAMATI ILIBAINI CHANGAMOTO ZIFUATAZO KATIKA SHIRIKA LA MAGAZETI ZANZIBAR.**

i. Kuwepo kwa Deni kubwa ambalo Shirika linazidai taasisi za Serikali jambo ambalo linazorotesha ukusanyaji wa mapato kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zilizopangwa. Shirika lilichukua hatua zifuatazo za kudai madeni hayo. Kwanza, Shirika liliandika  barua kwa taasisi zinazodaiwa na kufanya ufuatiliaji wa ana kwa ana, Pili lilifanya mkutano na wadai chini ya usimamizi wa PDB na kupata msaada wa kutolewa maagizo kutoka serikali kuu. Miongoni mwa maagizo hayo ni agizo la, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi alilolitoa tarehe 12 Februari, 2022 katika sherehe za maadhimisho ya miaka 20 ya Gazeti la ZanzibarLeo. Aidha, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi alizindikia barua Taasisi zote za Serikali  tarehe 21 Februari, 2022 yenye Kumbukumbu nambari BLM/57/MM/C.1/100 na Barua ya tarehe 07 Novemba, 2022 yenye kumbukumbu nambari BLM/57/MM/C.1/108 zinazozitaka taasisi kulipa deni wanalodaiwa na shirika la magazeti. Shirika liliiandikia barua Ofisi ya Rais Fedha na Mipango yenye kumbukumbu nambari SMS/M.2/VOL.11/33 ya tarehe 25 Julai, 2022 ili wazikate Taasisi hizo katika fedha zao za OC moja kwa moja ili kuepusha mrundikano na

engezeko la madeni hayo. Baada ya Jithada hizo, Baraza la Mapinduzi pia lilitoa agizo la kulitaka Shirika la Magazeti kupitia Wizara ya Habari kuwasilisha deni hilo Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ili Taasisi hizo ziweze kukatwa moja kwa moja katika OC zao. Barua kumbukumbu nambari BLM/19/HUM/C.1/89 ya tarehe 02 Mei 2023 kutoka kwa Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi Inahusika. Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ilitimiza agizo hilo kwa kuwasilisha deni hilo Ofisi ya Fedha na Mipango tarehe 12/05/2023 kwa barua yenye kumbukumbu nambari CAB.182/279/01/03/41. Hadi sasa bado agizo halijatekelezwa.

ii. Shirika kwa mwaka wa fedha 2023-2024 halikupangiwa kupatiwa fedha za ruzuku ya OC kusaidia uchapishaji wa magazeti.

iii. Kumekuwa na changamoto ya ucheleweji wa kupeleka magazeti kisiwani Pemba.

iv. Gharama kubwa za uchapishaji wa magazeti kutokana na shirika kukokuwa na mtambo wake wa kuchapishia magazeti na kupelekea shirika kuchapisha magazeti yake kwa kampuni binafsi.

v. Shirika la Magazeti linakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa jengo kwa sasa kutokana na kuongezeka wafanyakazi baada kuidhinishwa muundo wa Shirika.

vi. Shirika la Magazeti linakabiliwa na ukosefu wa baadhi ya wafanyakazi kwamba baadhi ya vitengo, divisheni na idara hadi sasa hazina watendaji na kupelekea kuwa na changamoto za kiutendaji wa kazi za Shirika. Katika kuitatua changamoto hii, shirika linaendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma kwa ajili ya kupatiwa watendaji

vii. Shirika linatakiwa kujiendesha kibiashara na kutoa huduma kwa umma kwa wakati mmoja japo ambalo litapelekea shirika kukosa ufanisi wa kiutendaji. Utatuzi wa changamoto hii ni shirika kuachiwa kufanya biashara moja kwa moja au kuhudumiwa ikiwa litaendelea kutoa huduma.

**MAONI YA KAMATI/USHAURI WA KAMATI**

i. Kamati inaishauri Wizara ya fedha na mipango iweze kutekeleza maagizo ya kukata deni kwa taasisi zinazo daiwa japo kwa asilimia kidogo ili shirika liweze kujiendesha pia kamati imeitaka Shirika kuendelea kujiimarisha kibiashara kwa kutumia mapato yake ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Shirika.

ii. Kamati inaiomba Serikali kuu kupitia Wizara kuendeleza jitihada ili kulipatia Shirika mtambo wa uchapishaji wa Magazeti ili kupunguza gharama za Uchapishaji pamoja na kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

iii. Kamati inalipongeza Shirika la Magazeti ya Serikali kwa kuchapisha na kusambaza habari kupitia mitandao ya kijamii kama vile youtube, Whatsap, Twitter, Instagram na Facebook. Pia kamati imelitaka shirika kuendeleza ubunifu katika usambazaji wa magazeti kwa njia mbali mbali.

iv. Aidha kamati inaishauri Wizazara kupitia Shirika kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ili kupunguza tatizo la wataalamu katika shirika la magazeti.

v. Kamati inapongeza Shirika kwa kuwa na toleo la kwanza la Sera ya ndani ya TEHAMA ambayo bado inaendelea kuboreshwa kwa ajili ya matumizi ya TEHEMA ya Shirika, Sera hiyo italisaidia Shirika kuendana na wakati uliopo sasa wa kutumia mifumo ya TEHAMA kwa shughuli zote za Shirika.

vi. Kamati inaipongeza wizara kupitia Shirika kwa kuchapisha nakala **3,000** za Jarida la Neema Zetu na kuzisambaza bure kwa wananchi kwa lengo la kuwahabarisha juu ya utekelezaji wa sera, mipango na mikakati ya serikali ya awamu ya nane.

**B. WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR (ZAGPA)**

Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar (ZAGPA) umeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Namba 12 ya mwaka 2018. Majukumu makuu ya Wakala ni kutoa huduma za uchapaji pamoja na uuzaji wa vifaa vya ofisi na vya kuandikia kwa

Taasisi za Serikali na Binafsi. Wakala wa Uchapaji unasimamiwa na Mkurugenzi Mtendaji ambaye huteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na anaawajibika kwa Bodi ya Wakurugenzi ya Wakala wa Uchapaji.

**CHANGAMOTO KATIKA WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR**

i. Uchakavu wa jengo la Wakala
ii. Ukosefu wa ofisi ya Wakala Pemba
iii. Ukosefu wa ghala la bohari kuu ya vifaa vya ofisi na kuanadikia
iv. Uhaba wa Fedha na Mtaji wa kuendesha Shirika.
v. Uhaba wa mitambo ya ya kisasa ya uchapishaji
vi. Upungufu wa Wataalam na mafundi wa mitambo ya Shirika.

**MAONI/USHAURI /MAPENDEKEZO YA KAMATI.**

i. Kamati inaishauri serikali kuikamilishia fedha za mradi wa ujenzi wa jengo jipya la ofisi za Wakala ili ujenzi huo uweze kukamilika kwa wakati.
ii. Kamati inaishauri Wakala wa Uchapaji kukopa ili iweze kujiendesha.
iii. Kamati inaishauri Wakala wa Uchapaji kuwalinda na kuwaenzi wateja wake waliorudi ili wasije kuwapoteza tena kwa kuimarisha huduma.
iv. Kamati inashauri Wizara wawapatie mafunzo baadhi ya watendaji wa shirika kwa kuwapeleka nchi jirani ili kupata mafunzo na uzoefu ili waje wamudu kuitumia vizuri mitambo itakayoletwa.
v. Kamati inaishauri Serikali kuwapatia ghala la kudumu Wakala wa Uchapaji ili kuondokana na changamoto ya kuhifadhia vifaa vyao pindi vinaposhushwa Bandarini.

**C. SHIRIKA LA UTANGAZAJI LA -ZBC**

Shirika la Zbc limeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Nam.4 ya mwaka 2013.Kabla ya kuanzishwa kwa Sherai hiyo shirika hili lilianzishwa kwa Tamko la Rais

(Presidential Decree), kwa hati ya kisheria nambari 111/2011.Baada ya kuanzishwa kwa sheria hiyo 2013, Shirika la ZBC likawa ni muunganisho wa Taasisi mbili ambazo ni Sauti ya Tanzania Zanzibar na Idara ya Televisheni (TVZ) ili kuifanya sekta ya Habari kwa Zanzibar kuwa ni chombo kimoja chenye nguvu.

**CHANGAMOTO ZA SHIRIKA LA UTANGAZAJI LA ZBC**

i. Uhaba wa wafanya kazi katika kituo cha utangazaji cha ZBC TV.
ii. Uhaba wa vitendea kazi na mitambo ya kisasa kama vile setelight
iii. Kutokuwepo kwa uzio katika kituo cha ZBC Pemba
iv. Uchakavu wa jengo kongwe Pemba ambalo linahitaji ukarabati kwa matumizi
v. Uhaba wa usafiri kwa Shirika.
vi. Kuwepo kwa muundo ambao hautambui uwepo wa nafasi ya Mkurugenzi wa Kituo cah ZBC Dar es Salam hali inayopelekea kukosa stahili na haki zake nyengine kwa mujibu wa Sheria.
vii. Uwepo wa Sheria ya ZBC Namb.4 ya mwaka 2013 ya muda mrefu ambayo imeonekana kuhitaji marekebisho.
viii. Kuwepo kwa mahitaji ya mapitio ya Kanuni za Sheria ya ZBC Namb.4 ya mwaka 2013.
ix. Uchakavu wa jingo la Utangazaji Rahaleo.
x. Uchakavu wa vitendea kazi na Samani za Ofisi Rahaleo.

**MAONI /USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI.**

a. Kamati inalipongeza Shirika la ZBC kwa kuwa na mabadiliko makubwa katika utekelezaji wa kazi zake licha ya kuwa na changamoto mbali mbali inazozikabili shirika hilo.
b. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara kuongeza nguvu katika ukarabati wa kituo cha utangazaji ili kituo hicho kiweze kuwa katika hali nzuri na kufanyakazi kwa ufanisi.

c. Kamati inaishauri Wizara kuharakisha kukamilisha uwepo wa Sheria mpya ya ZBC Namb.4 ya mwaka 2013 ambayo ni ya muda mrefu.
d. Kamati inaishauri serikali kwa kushirikiana na Tume ya Utumishi Serikalini kuwapatia kibali cha uwajiri kwa ZBC TV ili waweze kuwaajiri Wafanyakazi na waondokane na tatizo na uhaba wa wafanyakazi.
e. Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Tume ya utumishi serikalini kukamilisha kwa hatua zilizobaki marekebisho ya Mapendekezo ya Muundo mpya wa Shirika ili kuweza kutambua baadhi ya nafasi ambazo katika sheria hazikuwemo.
f. Kamati inaishauri Wizara kuharakisha ufanywaji wa mapitio ya kuwa na Kanuni za Sheria ya ZBC

## 2. PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Programu hii imeundwa na Programu Ndogo mbili ambazo ni Uimarishaji, Uhifadhi na Uendelezaji wa Utamaduni, Sanaa na Ubunifu pamoja na Ukuzaji na Uendelezaji wa Michezo Zanzibar ambapo kupitia Programu hii, huduma mbali mbali hutolewa kama vile Ukaguzi wa Filamu na Sanaa za Maonesho, Uendelezaji wa Matumizi Sahihi ya Kiswahili, Kusajili na Kusimamia Hakimiliki, Ukuzaji na Uendelezaji wa Michezo Zanzibar, Uimarishaji, Uhifadhi na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa Pamoja na Usimamizi wa Vyama vya Michezo.

Katika mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya Tanzania Shilingi 38,156,151,000/= zimepangwa kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

Kamati katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa Progaramu hii imeweza kutemblea taasisi mbali mbali ili kufahamu mafanikio na changamoto na kuweza kuishauri Serikali kama ifuatavyo:

## A. BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA ZANZIBAR

Baraza la Michezo la Taifa Zanzibar (BTMZ) limeanzishwa chini ya Sheria ya Baraza la Taifa la Michezo, Nambari 5 ya mwaka 2010. Miongoni mwa majukumu yake ya msingi ni kusajili na kusimamia vyama vya michezo pamoja na kukuza na kuendeleza michezo katika ngazi zote hapa Zanzibar.

Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar limeanzishwa chini ya Sheria nambari 5 ya mwaka 2010 na miongoni mwa majukumu ya msingi ni kusimamia vyama vya michezo vilivyosajiliwa pamoja na kukuza na kuendeleza mchezo katika ngazi zote hapa nchini. Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar linaongozwa na Katibu Mtendaji na lina jumla ya wafanyakazi 14 wakiwemo wanawake sita (6) na wanaume nane(8) kati ya hao Unguja kumi na moja (11) na Pemba watatu (3)

### CHANGAMOTO ZINAZOLIKABILI BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA ZANZIBAR.

(a) Uhaba wa fedha na wafadhili unaopelekea kushindwa kutekeleza shughuli zilizopangwa kwa ufanisi.

(b) Ufinyu na uchakavu wa Ofisi ya Baraza.

(c) Ukosefu wa usafiri wa kudumu wa ufuatiliaji wa kazi za kila siku za Baraza.

### MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

(a) Kamati inaishauri Wizara kulipatia Baraza la Michezo Zanzibar nafasi katika viwanja vipya vya Amani Complex ili chombo hicho kiweze kuwa na ofisi rasmi ya kutekeleza vyema shughuli za kuendeleza sekta ya michezo kwa ufanisi.

(b) Kamati inaupongeza Uongozi wa Wizara kwa kuhakikisha kuwa sekta ya michezo inaendelezwa pamoja na kukuza vipaji kwa vijana ili waweze kujitegemea na kujiajiri wenyewe bila ya kutegemea ajira kutoka Serikalini

(c) Kamati inaishauri Serikali kuliongezea bajeti Baraza la Michezo la Taifa kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Baraza pamoja uendeshaji wa shughuli za

Michezo kwani hivi sasa Baraza limekuwa likishindwa kutekeleza vyema majukumu yake.

(d) Kamati inaishauri Serikali katika bajeti ya mwaka 2024/2025 kuitengea fedha kwa ajili ya ununuzi wa gari ya kudumu ya Baraza la Michezo la Taifa ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi.

(e) Kamati inaishauri Wizara kupitia Baraza la Michezo kwa kuzisimamia kwa karibu kamati maalum ya kubuni vyanzo mbadala vya mapato ya kuendeshea shughuli za Baraza pamoja na kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo viongozi wa vyama vya michezo yanayohusiana na utafutaji masoko katika michezo sambamba na kuendelea kuvisaidia vyama vya michezo katika kutafuta ufadhili.

(f) Kamati inalipongeza Baraza la Michezo kwa kushirikiana na Kampuni ya Tosh Sports Promotion kufanikisha kwa mara ya kwanza kuandaa mashindano ya mchezo wa ngumi yaliyofanyika katika Uwanja wa Mao Ze Dong tarehe 27/08/2023,Pambano ambalo lilishirikisha Mabondia kutoka Tanzia Bara na Zanzibar.

(g) Aidha Kamati inalipongeza Baraza kwa kufanikisha kufanyika kwa chaguzi za vyama ambavyo vilikuwa havijafanya chaguzi kwa muda mrefu. Vyama vyenyewe ni Chama cha Riadha, Handball, Judo, Trithlon, Taekwondo WTF na Mpira wa vinyoya. Hatua hiyo itasaidia kutambua rasmi uongozi wa vyama hivyo katika utekelezaji wa majukumu yao.

(h) Aidha Kamati imeridhika na kazi za Baraza Baraza kwa kufufua upya mchezo wa Trithlon ambao ulisita kufanya shughuli zake kwa kipindi kirefu. Chama cha Mchezo huu ni miongoni mwa vyama vichache vya michezo vya Zanzibar vyenye uanachama katika mashirikisho ya michezo ya kimataifa.

**B. BARAZA LA SANAA, SENSA YA FILAMU NA UTAMADUNI**

Baraza la Sanaa, sensa ya filamu na Utamaduni (BASSFU) limeanzishwa kwa mujibu wa sheria namb.7 ya mwaka 2015. Baraza lina jukumu la kuhakikisha

kuwa pamoja na mambo mengine filamu zinazoanzishwa nchini zinahakikiwa ili kulinda mila, silka na desturi za mzanzibar.

**CHANGAMOTO ZA BARAZA LA SANAA SENSA YA FILAMU NA UTAMUDUNI**

a) kukosekana kwa usafiri wa uhakika wa kufanyia ufuatiliaji wa kila siku wa kazi za baraza.
b) ufinyu wa ofisi
c) uchache wa wafanyakazi Afisi ya Baraza Pemba.
d) Ukosefu wa Bajeti.
e) Uchakavu wa samani za Ofisi.

**MAONI YA KAMATI/USHAURI WA KAMATI**

a) Kamati inaishauri wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa kushirikiana na Wizara fedha na Mipango kuhakikisha kuwa Baraza la Sanaa, Sensa, Filamu na Utamaduni inapatiwa gari ya kudumu kwa ajili ya kufanya shughuli zao za kila siku.
b) Kamati pia inaishauri wizara ya Habari kuwapatia afisi kubwa na nzuri ambayo itasaidia kufanya kazi zao kwa ufanisi.
c) Kamati inaishauri Serikali kuwapatia kibali baraza la Sanaa, Sensa, Filamu na Utamaduni ili waweze kuajiri wafanyakazi katika ofisi ya Pemba ili na waondokane na tatizo la uhaba wa wafanya kazi.

**C. ZIARA YA KAMATI KATIKA Mradi wa Ukarabati wa Uwanja wa Amaani- Unguja**

Katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2023 Wizara inaendelea na utekelezaji wa Uimarishaji wa miundombinu ya michezo Zanzibar. Mradi wa Ukarabati wa Uwanja wa Amani Unguja na Mradi wa Ukarabati wa Uwanja wa Gombani Pemba inatekelezwa na imefikia katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mradi wa Ukarabati wa Uwanja wa Amaan Unguja ni Mradi uliotekelezwa kwa fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa lengo la kuuboresha na kuufanya

kuwa wa kisasa na wenye kukidhi viwango vya Kimataifa. Wizara ilitekeleza Mradi huu kupitia Mkandarasi ambaye ni **Kampuni ya Orkun** kwa thamani ya dola za Kimarekani 22.1. Katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2023 jumla ya dola za kimarekani milioni 12 zimelipwa, na jumla ya fedha zote zilizolipwa katika mradi ni dola za kimarekani milioni 18 sawa na asilimia 81.4.

Mradi huu ulijumuisha ukarabati wa kiwanja cha mpira, ujenzi wa majukwaa, mifumo ya maji na umeme, ujenzi wa minara ya taa, ujenzi wa viwanja viwili vya mpira wa miguu vya nje, viwanja vya ndani vya michezo midogo midogo, ukumbi wa kuchezea judo, ukarabati wa hoteli, eneo la kuegesha magari na ujenzi wa mikahawa na maduka. Utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 98 na unatarajiwa kukamilika mwanzoni mwa mwezi machi 2024 baada ya mkandarasi kuongezewa muda wa miezi mitatu.

**CHANGAMOTO ZA MRADI WA UKARABATI UWANJA WA AMANI**

a) kuchelewa kuingizwa fedha ili kuweza kukamilisha maeneo zaidi ya miradi
b) kukosekana kwa vipoza hewa katika viwanja vya judo na viwanja vya ngumi.

**MAONI YA KAMATI/USHAURI KWA UWANJA WA AMANI**

c) Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha viwanja vipya vya AMANI COMPLEX vinatuzwa na kuenziwa ili kuweza kutumika katika shughuli za michezo ya kitaifa na kimataifa.
d) kamati inaishauri Wizara ya Fedha kuingiza kwa wakati fedha za miradi ili ipate kumaliza kwa wakati uliopangwa
e) kamati inaishauri Wiazara ya Habari Vijana Utamaduni na Michezo kuhakikisha kuwa katika viwanja vyote vya ngumi vinatiwa vipoza hewa ili watu ambao wanaenda kuangalia michezo hiyo basi wanakuwa katika hali nzuri na salama.

f) Kamati pia inaishauri Wizara kutafuta kampuni zenye uwezo nzuri wa kufanya usafi ili kujenga mazingira bora ya usafi katika viwanja hivyo.
g) Kamati inaipongeza Wizara kwa kazi kubwa ya kusimamia shughuli za ujenzi wa viwanja vya Amani hadi kufikia hatua iliyofiwa.

**A.Mradi wa Ukarabati wa Uwanja wa Gombani Pemba**

Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na umeanza utekelezaji wake katika mwaka wa fedha 2022/2023. Wizara inatekeleza mradi huu kupitia Kampuni ya Ujenzi ya **SALIM CONSTRUCTION LTD JV OSAJU COMPANY LTD** kwa bajeti ya **shilingi 5,600,427,326/-.** Katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2023 kiasi cha **shilingi 1,675,778,484/-** zimelipwa kwa mkandarasi na kufanya jumla ya fedha zote zilizolipwa katika mradi kufikia **shilingi 3,428,349,400/-** sawa na asilimia **61.2** kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi.

Lengo la mradi huu nikuuboresha uwanja wa Gombani kutokana na hali mbaya ya uchakavu. Mradi huu unajumuisha ujenzi wa Minara na kubadilisha Taa, kubadilisha milango na madirisha, kubadilisha mifumo ya maji na umeme, ukarabati wa vyoo, uwekaji wa nyasi bandia, uwekaji wa tatan katika eneo la kukimbilia, ukarabati wa majukwaa ya watazamaji, ukarabati wa vyumba na majukwa ya watu mashuhuri, na upakaji wa rangi eneo lote la ndani na nje ya uwanja.

Utekelezaji wa mradi huu umefikia **asilimia 95** na unatarajiwa kukamilika mwanzoni mwa mwezi machi 2024 baada ya mkandarasi kuongezewa muda.

**CHANGAMOTO ZA UKARABATI NA UBORESHAJI WA UWANJA WA GOMBANI PEMBA**

i. kuchelewa kuingizwa fedha ili kuweza kukamilisha maeneo zaidi ya miradi
ii. Kuchelewa kukamilika kwa wakati katika baadhi ya maeneo
iii. Kuongezeka kwa gharama za awali za mradi(Variation) kutokana na kuongezeka kwa baadhi ya huduma zinazohitajika ambazo zilikosa kuzingatiwa katika makaubalainao ya awali.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

i. Kamati inaishauri Wizara husika inayosimamia masuala ya fedha kuhakikisha inakamilisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kukamilisha kazi ya mradi iliyobaki.
ii. Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha inasimamia vyema awamu iliyobaki ili kazi ya uimarishaji wa viwanja vya Gombani iweze kukamilka.
iii. Kamati inapendekeza kutumiwa wataalamu wetu wa miradi katika miradi ya serika tokea mwanzoni mwa uwandaaji wa mradi ili kuepuka kuongezeka kwa gharama zisizo za lazima (Variation).
iv. Kamati inashauri uwanja uwekewe uzio ili kuepusha uharibifu wa Uwanja huo.
v. Kamati pia inaishauri Wizara kutafuta kampuni zenye uwezo nzuri wa kufanya usafi ili kujenga mazingira bora ya usafi pindipo kiwanja hicho kikikamilika.

**3. PROGARAMU KUU YA MAENDELEO YA VIJANA (PJ0302**

Lengo kuu la Programu hii ni kuratibu shughuli za maendeleo ya vijana, kuwawezesha kwa kuwajengea uwezo ili kuimarika kiuchumi, kijamii na kisiasa kupitia progaramu mbali mbali.

Katika mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya Tanzania Shilingi 628,598,000/= zimepangwa kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

**CHANGAMOTO**

- Uimarishaji wa shughuli za Maendeleo ya Vijana na kuwatafutia vijana fursa mbali mbali kwa kuwaunganisha na washirika wa Maendeleo ya Vijana.
- Ukosefu wa fedha unaopelekea mabanda ya Ole kutoendelezwa.

**MAONI/USHAURI WA KAMATI**

- Kamati inaipongeza Wizara kwa kukamilisha kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2023 .
- Kamati inaishauri kuwa na mipango endelevu ya muda mfupi na mrefu ya uimarishaji wa shughuli za Maendeleo ya Vijana na kuwatafutia vijana fursa mbalimbali kwa kuwaunganisha na washirika wa Maendeleo ya Vijana.
- Kuviendeleza vituo vya Bweleo, Weni, Kangagani kwa kuweka vifaa na kuweka Walimu wa kuviendeleza na kutoa taaluma stahiki ili vijana waweze kujiajiri.

**4. PROGRAMU KUU YA UTAWALA NA UENDESHAJI WA WIZARA(PJ0304)**

Kiujumla utekelezaji wa Programu Kuu hii unajumuisha Programu Ndogo Tatu nazo ni Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Tafiti, Programu Ndogo ya Utumishi na Uendeshaji na Programu Ndogo ya Uratibu wa Wizara Ofisi Kuu Pemba.

Katika mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya Tanzania Shilingi 3,542,926,000/= zimepangwa kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO**

1. Upatikanaji mdogo wa fedha za uendeshaji wa Ofisi. Changamoto hii hupelekea kutokufikia malengo ya utekelezaji wa mpango kazikwa mwaka wa bajeti husika.
2. Vyama vya Michezo kutegemea kwa asilimia mia moja (100) ruzuku kutoka Serikalini katika kuendesha shughuli zao.
3. Kuwepo kwa mrundikano wa madeni makubwa na ya muda mrefu kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar, Shirika la Magazeti ya Serikali pamoja na Shirika la Utangazaji Zanzibar kwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, yanayotokana na huduma mbali mbali kama vile uchapaji, utangazaji wa matangazo, urushaji wa vipindi, usambazaji wa magazeti kwa Serikali na Taasisi Binafsi n.k.
4. Wizara kuwa na majengo chakavu na kutokuwa na nafasi ya kutosha kwa ajili ya wafanya kazi na watu wanokuja kupata huduma
5. Baadhi ya taasisi zinamrundikano mkubwa wa watendaji jambo ambalo halileti ufanisi katika utendaji wa kazi.
6. Vyama vya michezo kushindwa kujiendesha vyenyewe na hivyo kuitegemea Wizara kwa asilimia mia moja, Serikali iwatengee bajeti maalum kwa ajili ya shughuli za utawala na uendeshaji kwa vyama hivyo.
7. Uchache wa vyombo vya usafiri kwa Taasisi zilizopo chini ya Wizara, jambo ambalo linapelekea kushindwa kutekeleza majukumu ya ufuatiliaji wa kazi za ofisi.
8. Uhaba wa Miundombinu ya Michezo na Sanaa. Wizara kwa sasa inaendelea na jitihada za kujenga miundo mbinu mipya na mizuri ya michezo

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inapendekeza kwa Serikali kusimamia uamuzi uliotolewa na Baraza la Mapinduzi juu ya suala zima la kulipwa kwa madeni wanayodai kwa baadhi ya Taasisi za Serikali na Binafsi ili Taasisi hizo ziweze kujiendesha wenyewe bila ya kutegemea fedha kutoka Serikali.

(b) Kamati inaipongeza Wizara kwa kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa uzalendo mkubwa na ubunifu licha ya uhaba wa rasilimali watu na fedha.

(c) Kamati inaishauri Serikali kulitafutia ufumbuzi wa Upatikanaji mdogo wa fedha za uendeshaji wa Ofisi kwa karibu taasisi nyingi za umma ili taasisi hizo ziweze kufanyakazi kwa ufanisi.

(d) Kamati inaishauri Wizara kuendelea na juhudi na mchakato wa kutafuta ufadhili kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la ofisi.

(e) Kamati inaishauri Serikali kutenga bajeti maalum kwa ajili ya shughuli za utawala na uendeshaji kwa vyama vya michezo.

(f) Kamati inaipongeza wizara kwa kusimamia mageuzi makubwa na jitihada za kujenga miundo mbinu mipya na mizuri ya michezo

(g) Aidha Kamati inaipongeza Wizara kwa kukamilisha kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2023 ambapo tayari imeshazinduliwa tarehe 15, Disemba 2013 na Mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla Makamo wa Pili wa Rais Zanzibar. Sambamba na Sera mpya ya Habari ya mwaka 2023 kuwepo katika hatua ya kuchapishwa na hatimae kuzinduliwa. Pia, Wizara inaendelea na hatua mbalimbali za kuzifanyia mapitio sera ya Tume ya Utangazaji 2008, Sera ya Utamaduni 2005 s na kuandaa Sera mpya ya Kiswahili na Sera ya Filamu.

# SEHEMU YA SITA

## 6.0 HITIMISHO

Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi inawapongeza kwa dhati Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Manaibu Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wote kwa ujumla wa Wizara zote Nne zinazosimamiwa na Kamati hii kwa mashirikiano makubwa waliyoipatia Kamati kwa kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake ya Kikatiba na Kikanuni.

Kamati kwa upekee inazipongeza Wizara zetu ya Elimu na Afya kwa kuiwezesha Kamati kufanya ziara za kuijengea uwezo Kamati kwa upande wa Tanzania Bara. Kwa kweli Kamati ya Ustawi wa Jamii imeweza kujifunza mengi yanayohusu taasisi za wizara hizo huko Tanzania Bara na kupata uwelewa mkubwa kuhusu mafanikio na changamoto za taasisi hizo katika utekelezaji wa kazi zake na kuweza kuishauri Serikali.

Aidha, Kamati inatoa shukurani za kipekee kwa Maafisa Wadhamini wa Wizara hizi zote pamoja na wasaidizi wao wote kwa mashirikiano mazuri waliyoipatia Kamati wakati wote Kamati inapokuwa Pemba katika kutekeleza majukumu yake.

Kamati inampongeza Mhe. Spika wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Zubeir Ali Maulid na uongozi wote wa Baraza pamoja na wafanyakazi wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha vyema Kamati kutekeleza majukumu yake na kuweza kutayarisha Ripoti yake kwa mwaka 2023/2024. Kamati inashauri mashirikiano hayo yaendelezwe kwa kipindi chote kinachofuata.

Mwisho kabisa na kwa umuhimu mkubwa Kamati inawapongeza kwa dhati kabisa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2025